

MUHTASARI WA RIPOTI YA DUNIA YA UFUATILIAJI WA ELIMU

2021/2

Wahusika wasio wa serikali katika elimu

NI NANI ANAYECHAGUA? NI NANI ANAYEPOTEZA?

unesco

Sustainable Development Goals

Global Education Monitoring Report

MUHTASARI WA RIPOTI YA DUNIA YA UFUATILIAJI WA ELIMU

2021/2

Wahusika wasio wa serikali katika elimu

NI NANI ANAYECHAGUA? NI NANI ANAYEPOTEZA?

Azimio la Incheon la elimu la 2030 na Mfumo wa Utekelezaji zinabainisha kuwa mamlaka ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu ni kuwa "utaratibu wa kufuatilia na kuripoti juu ya Lengo nambari 4 katika Maendeleao Endelevu (SDG 4) na juu ya elimu katika malengo mengine". Wajibu wake ni "kuripoti kuhusu utekelezaji wa mikakati ya kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha kuwa washirika wote husika wanatimiza ahadi zao kama sehemu ya ufuatiliaji na ukaguzi wa jumla wa malengo ya SDG". Ripoti hii imeandaliwa na timu ya kujitegemea kwa ushirikiano na UNESCO.

Majina yaliyotumika na uwasilishaji wa maudhui katika chapisho hili hayawasilishi maoni yoyote ya UNESCO kuhusiana na sheria ya nchi, taifa, jiji au eneo lolote lile, au mamlaka yake, au kuhusiana na uwekaji mipaka yake.

Wajumbe wa timu hii wanawajibika kwa uchaguzi na uwasilishaji wa ukweli na maoni yaliyo katika kitabu hiki, ambayo si lazima yawe yanaambatana na yale ya UNESCO na UNESCO haiwajibiki. Mkurugenzi wake anawajibika kwa mawazo na maoni yaliyotolewa katika Ripoti hii.

Timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu

Mkurugenzi: Manos Antoninis

Daniel April, Bilal Barakat, Marcela Maria Barrios Rivera, Madeleine Barry, Katherine Black, Nicole Bella, Celia Eugenia Calvo Gutierez, Daniel Caro Vasquez, Anna Cristina D'Addio, Dimitra Dafalia, Dmitri Davydov, Francesca Endrizzi, Constanza Ginestra, Chandni Jain, Priyadarshani Joshi, Maria-Rafaela Kaldi, Josephine Kiyenje, Craig Laird, Katie Lazaro, Kate Linkins, Camila Lima De Moraes, Kassiani Lythrangomitis, Anissa Mechtar, Claudine Mukizwa, Yuki Murakami, Manuela Pombo Polanco, Judith Randrianatoavina, Kate Redman, Maria Rojnov, Laura Stipanovic, Ulrich Janse van Vuuren, Juliana Zapata, Lema Zekrya na Jiaheng Zhou.

Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu ni toleo huru linalochapishwa kila mwaka. Ripoti hii imegharamiwa na muungano wa serikali mbalimbali, taasisi za kimataifa na mifuko binafsi na kuwezeshwa na UNESCO.

Ripoti hii inapatikana kwa kila mtu chini ya leseni ya IGO (CC-BY-SA 3.0 IGO) ya Attribution-ShareAlike 3.0 (http://creativecommons.org/licenses/by-sa/3.0/igo/). Kwa kutumia maudhui yaliyo ndani ya ripoti hii, watumiaji wanakubali kutii masharti ya matumizi ya UNESCO Open Access Repository (http://www.unesco.org/open-access/terms-use-ccbysa-en).

Leseni ya sasa inasimamia sehemu ya maandishi pekee. Ili kutumia nyenzo yoyote ambayo haijabainishwa kuwa inamilikiwa na UNESCO, anayetaka kutumia atahitaji kuomba ruhusa mapema kutoka: publication.copyright@unesco.org au UNESCO Publishing, 7, place de Fontenoy, 75352 Paris 07 SP Ufaransa.

Leseni ya sasa inasimamia sehemu ya maandishi pekee. Ili kutumia picha, unahitaji kuomba ruhusa mapema. UNESCO ni Mchapishaji Huru na machapisho yote yanapatikana mtandaoni, bila malipo kupitia hazina ya hati ya UNESCO. Mauzo yoyote ya machapisho yanayofanywa na UNESCO ni kwa ajili ya kulipia gharama ya uchapishaji au unakili wa maudhui haya kwenye karatasi au kanda za CD, au usambazaji. Lengo si kupata faida.



Kichwa asili kwa Kiingereza: *Global Education Monitoring Report* Summary 2021/2022: Non-state actors in education: Who chooses? Who loses?

Ripoti hii inaweza kutajwa kama: UNESCO. 2021. *Global Education Monitoring Report* Summary 2021/2022: Non-state actors in education: Who chooses? Who loses? Paris, UNESCO.

Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na:
Timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu
UNESCO, 7, place de Fontenoy
75352 Paris 07 SP, France
Barua pepe: gemreport@unesco.org
Simu.: +33 1 45 68 07 41
www.unesco.org/gemreport

Makosa yoyote ya kiuchapishaji au kuondolewa kwa baadhi ya maneno yatarekebishwa kwenye toleo litakalowekwa kwenye tovuti ya www.unesco.org/gemreport

© UNESCO, 2022
Haki zote zimehifadhiwa
Toleo la pili
Lilichapishwa 2021 na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni
7, Place de Fontenoy, 75352
Paris 07 SP, Ufaransa

Mpangilio wa uchapishaji umefanywa na UNESCO
Ubunifu wa vielelezo umefanywa na Optima Graphic Design Consultants Ltd
Mpangilio umefanywa na Apricot Business Solutions

Picha ya jalada: Jaap Joris Vens / Super Formosa Photography
Nukuu: Njia tofauti za kufika shuleni, Uholanzi.

Michoro imefanywa na Housatonic
Vibonzo na Julio Carrión Cueva (Karry) na Miguel Morales Madrigal

Msururu wa Ripoti ya Ufuatiliaji wa Elimu Duniani

2021/2	Wahusika wasio wa serikali katika elimu: Ni nani anayechagua? Ni nani anayepoteza?
2020	Ujumuishaji na elimu: Tukisema wote, basi ni wote
2019	Uhamiaji, ufurushwaji na elimu: Kuunganisha jamii badala ya kuigawanya
2017/8	Uwajibikaji katika elimu: Kutimiza ahadi zetu
2016	Elimu kwa ajili ya watu na dunia: Kujenga hatima endelevu kwa wote

Msururu wa EFA wa Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu

2015	Elimu kwa Wote 2000-2015: Mafanikio na changamoto
2013/4	Kufundisha na kujifunza: Kufanikisha ubora kwa wote
2012	Vijana na stadi: Kufanya elimu yenye manufaa kwa kazi
2011	Mgogoro ulifichika: Mapambano ya silaha na elimu
2010	Kuzifika jamii zilizoko pembezoni
2009	Kuushinda ubaguzi: Umuhimu wa utawala bora
2008	Elimu kwa Wote kufikia 2015: Je, tutaweza?
2007	Msingi Imara: Maelezi na elimu ya awali
2006	Kusoma, kuandika na kuhesabu kwa ajili ya maisha
2005	Elimu kwa Wote: Ubora ni kigezo
2003/4	Jinsia na Elimu kwa Wote: Kuelekea usawa
2002	Elimu kwa Wote: Je, dunia inafuata mwelekeo sahihi?

Ripoti hii na maudhui yote yanazohusiana yanaweza kupakuliwa hapa: http://bit.ly/2021gemreport

ED-2021/WS/38



Wahusika wasio wa serikali katika elimu 1

Ujumbe Muhimu 1

Msaada wa kifedha katika elimu ya umma ni imara 3

Hoja tofauti huendesha mjadala wa kuunga mkono au kupinga utoaji wa elimu usio wa serikali. 3

Visasili kuhusu wahusika wa serikali na wasio wa serikali katika elimu hutawala 5

Utoaji wa Elimu 9

Usimamizi na udhibiti 10

Fedha 11

Ushawishi 13

Utunzaji na elimu ya chekechea 14

Elimu ya juu 15

Elimu ya kiufundi na ya watu wazima 16

Mapendekezo 17

Ufuatiliaji wa elimu katika Malengo ya Maendeleo Endelevu 22

Nchi zimewasilisha vigezo teule vya kitaifa vya lengo la 4 la malengo endelevu 22

COVID-19 23

Lengo la 4.1. Elimu ya msingi na ya sekondari 25

Lengo la 4.2. Elimu ya chekechea 26

Lengo la 4.3. Elimu ya kiufundi, ya juu na ya watu wazima 27

Lengo la 4.4. Ujuzi wa kazi 28

Lengo la 4.5. Usawa 28

Lengo la 4.6. Kujua kusoma, kuandika na kuhesabu 29

Lengo la 4.7. Maendeleo endelevu na uraia wa kimataifa 30

Lengo la 4.a. Vistawishi vya elimu na mazingira ya kujifunza 30

Lengo la 4.b. Ufadhili 31

Lengo la 4.c. Walimu 31

Elimu katika Malengo Mengine ya Maendeleo Endelevu 32

Ufuatiliaji wa Fedha 32



PICHA: UNICEF/ Olivie Asseli

Wahusika wasio wa serikali katika elimu

UJUMBE MUHIMU

Hakuna sehemu yoyote ya elimu ambayo wahusika wasio wa serikali hawashirikishwi.

Kwa ufupi, bila wahusika wasio wa serikali elimu ya watoto milioni 350 zaidi ingekuwa jukumu la serikali. Lakini kushirikisha wahusika wasio wa serikali pia huathiri vitabu vya kiada wanavyotumia, chakula katika maduka ya shule, msaada wa ziada wanaopata, ujuzi wanaojifunza na mengine mengi.

Watu wengi wanaunga mkono elimu ya umma.

Watu watatu kati ya wanne katika nchi 34 za kipato cha kati na cha juu wangependelea serikali iwekeze zaidi katika elimu. Msaada unavyoongezeka, ndivyo nchi inavyoendelea kukosa usawa. Takriban watu tisa kati ya kumi wanaonelea elimu kimsingi inapaswa kuwa ya umma.

Lakini maoni haya yameendelea kupungua katika nchi kadhaa za kipato cha chini na cha kati.

Ambapo shule za umma zilikuwa chache na ubora wake ulikuwa umezorota, familia nyingi ziliamua kuonyesha msimamo wao kwa kujiondoa. Idadi ya taasisi za binafsi duniani kote iliongezeka kwa asilimia 7 katika kipindi cha miaka 10: na kufika asilimia 17 kufikia mwaka 2013 katika elimu ya msingi na asilimia 26 kufikia mwaka 2014 katika elimu ya sekondari. Tangu wakati huo, idadi hiyo haijabadilika. Katika Asia ya Kati na ya Kusini idadi ya waliojiandikishaji katika taasisi za binafsi ni asilimia 36 katika elimu ya msingi na asilimia 48 katika elimu ya sekondari.

Elimu ya umma si ya bure.

Kaya huchangia asilimia 30 ya jumla ya matumizi ya elimu ulimwenguni na asilimia 39 katika nchi zenye kipato cha chini na cha kati. Mojawapo ya sababu ni kutokana na familia tajiri kujaribu kuwapa watoto wao nafasi ya ushindani. Lakini sehemu kubwa inatumika kwa elimu ya chekechea, ya msingi na ya sekondari ambazo serikali iliahidi kutoa bure. Takriban asilimia 8 ya familia hukopa ili kulipia elimu, asilimia inayopanda hadi 12 katika nchi za kipato cha chini na asilimia 30 au zaidi huko Haiti, Kenya, Ufilipino na Uganda.

Elimu ya umma mara nyingi huwa haijumuishi wote.

Mifumo mingi ya elimu ya umma hushindwa kuzuia utabakishaji na ubaguzi. Ripoti ya utofauti wa kijamii katika shule, kulingana na Programu ya Takwimu za Tathmini ya Wanafunzi wa Kimataifa, iligundua kuwa Argentina, Brazil, Chile na Meksiko zilikuwa na viwango sawa vya juu vya utabakishaji katika 2018, ingawa Chile sanasana hukosolewa kwa kuwa na idadi kubwa ya taasisi za binafsi katika mfumo wake.

Hakuna aina moja ya mtoa huduma anayetoa elimu bora kuliko mwingine yeyote.

Takwimu kutoka nchi 30 za kipato cha chini na cha kati zinaonyesha kuwa, mara tu sifa za kaya zinapozingatiwa, thamani dhahiri inayotokana na kuhudhuria shule ya binafsi hupungua kwa nusu hadi theluthi mbili. Katika sampuli ya nchi 49, uwezekano wa matajiri kwenda shule za binafsi ni karibu mara kumi zaidi ya ule wa maskini. Na wazazi ambao wanaweza kuchagua shule hufanya hivyo kwa sababu za imani za kidini, urahisi wa kufika pale na sifa za kidemografia za wanafunzi badala ya ubora, ambao mara nyingi huwa hawana habari za kutosha.

Uwezo wa kudhibiti, kufuatilia na kutekeleza huwa chini ambapo mahitaji yako juu.

Uchambuzi wa mifumo 211 ya elimu kwa ajili ya wavuti ya PEER unaonyesha kuwa kanuni huwa zinazingatia usajili, idhini au leseni (asilimia 98), vyeti vya ualimu (asilimia 93), miundombinu (asilimia 80) na uwiano wa wanafunzi/walimu (asilimia 74). Kanuni zina uwezekano mdogo wa kuzingatia ubora au usawa: asilimia 67 hudhibiti uamuzi wa ada, asilimia 55 huzuia taratibu baguzi za uandikishaji wa wanafunzi katika shule zisizo za serikali, asilimia 27 hupiga marufuku kutengeneza faida na ni asilimia 7 pekee zenye vipimo vinavyosaidia ufikiaji wa vikundi visivyojiweza. Ukufunzi wa binafsi haudhibitiwi katika asilimia 48 ya nchi na unadhibitiwa tu katika sheria za kibiashara katika asilimia 11 ya nchi.

Wahusika wasio wa serikali wapo zaidi katika elimu ya chekechea, ya kiufundi, ya juu na ya watu wazima.

Wakati mwingine hali hii huathiri usawa na ubora. Kwa jumla, gharama ya juu ya elimu ya chekechea na ile ya juu ambayo haitolewi na serikali inamaanisha kuwa wengi katika taasisi hizo ni watu wa matabaka ya juu kutoka mijini. Nchini Marekani, vyuo vikuu vinavyozingatia uongezaji wa faida vimehusishwa na kuzorota kwa matokeo ya wanafunzi. Taasisi zinazotoa mafunzo ya kibinafsi kupitia ushindani wa soko au mifumo ya kukuza ujuzi, kama vile mpango wa mkopo wa TVET FEE-HELP wa Australia na Shirika la Kitaifa la Kukuza Ujuzi la India, zililazimika kufikiria upya michakato ya uwajibikaji na ufuatiliaji ili kuongeza ubora wa utoaji wa elimu wa binafsi na kuboresha matokeo ya kuajiriwa.

Serikali zinahitaji kuona taasisi zote za elimu, wanafunzi na walimu kama sehemu ya mfumo mmoja.

Viwango, habari, vichochezi na uwajibikaji vinapaswa kusaidia serikali kulinda, kuheshimu na kutimiza haki ya elimu kwa wote na vinapaswa kuzizuia zisikose kushughulikia masuala ya upendeleo au unyonyaji. Si lazima elimu inayofadhiliwa na umma itolewe hadharani, lakini utofauti katika michakato ya elimu, matokeo ya wanafunzi na mazingira ya kazi ya walimu yanapaswa kushughulikiwa moja kwa moja. Ufanisi na uvumbuzi havipaswi kuwa siri ya kibiashara; badala yake, vinapaswa kutangazwa na kutekelezwa na wote. Ili kufanikisha hilo, uwazi na uadilifu katika mchakato wa sera ya elimu ya umma vinahitaji kudumishwa.

Sio kila wakati ambapo serikali zimeongoza elimu. Kihistoria, elimu iliandaliwa bila mpangilio na kwa njia zisizo rasmi na dini, familia na chama. Kuanzia mwishoni mwa karne ya 18, mataifa yaliona fursa ya kukuza uchumi wao kupitia wafanyakazi walioelimika na kukuza na kuimarisha utambulisho wa kitaifa kupitia shule za umma. Serikali zilikuwa tayari kulipia gharama kubwa ya kutoa huduma hii ya umma kwa sababu ya faida kubwa kwa jamii na uchumi. Kwa nchi zilizokuwa zimepata uhuru katika karne ya 20, kujenga mfumo wa elimu ya umma kulikuwa alama ya ukombozi kutoka kwa ukoloni. Elimu ya umma daima ililenga kukuza maadili mema au itikadi tawala. Miundo mipya ilipita na ikachukua nafasi ya miundo ya jadi ya elimu.

Hata hivyo elimu pia ni bidhaa ya kibinafsi. Kupata elimu zaidi huboresha fursa za mtu binafsi na kunaweza kuwatenga wengine wasipate fursa hizo. Wale wanaoweza kupanda ngazi ya elimu wana nafasi nzuri ya kufikia kiwango cha juu cha maisha na faida kubwa. Kwa kuwa mifumo ya elimu haiwezi kumudu kila mtu katika ngazi za juu, familia zinafanya kila ziwezalo kuhakikisha kuwa watoto wao ndio wanaofika kileleni. Ushindani kama huo huzalisha mahitaji, ambayo kwa upande wake husababisha usambazaji wa bidhaa na huduma za elimu. Kulingana na muktadha na muundo wa kitaifa, masoko yanaweza kuibuka katika utoaji wa moja kwa moja wa huduma za elimu ambazo zinaleta faida.

MSAADA WA KIFEDHA KATIKA ELIMU YA UMMA NI IMARA

Machaguo ya elimu huamua maisha ya watoto. Wazazi hawapaswi tu kufanya mahesabu rahisi ya gharama na faida za kifedha lakini pia kuzingatia mambo mengi, yanayohusiana. Machaguo kuhusu kile kinachofundishwa, jinsi kinavyofundishwa, na nani na wapi huonyesha maoni shindani ya ulimwengu na matarajio ya wazazi na ya wadau wengine wa elimu. Machaguo haya yanahusu vipimo viwili vikuu: udhibiti na usambazaji wa rasilimali, na maadili na imani kwa ajili ya kubadilisha jamii. Machaguo ya elimu yanaathiriwa sana na siasa na hudhihirika kwa njia wazi au zisizo wazi katika ajenda za kisiasa. Mbali na sababu za kibinafsi za kiitikadi na za kawaida, uelewa wa changamoto za kijamii na jinsi serikali, watu na taasisi zinapaswa kuhusiana hutofautiana kati ya nchi. Uelewa huu huathiri mitazamo juu ya sera ambazo serikali inapaswa kufuatilia na zinafaa kumfaidi nani.

Utafiti juu ya msaada kwa elimu ya umma unafanywa zaidi na nchi zenye mapato ya juu. Utafiti wa hivi karibuni wa mitazamo nchini Denmaki, Ufaransa, Ujerumani, Ayalandi, Italia, Uhispania, Uswidi na Uingereza ulionyesha kuwa wahojiwa walipoulizwa wapatie kipaumbele moja ya maeneo nane ya matumizi ya ziada, elimu ilikuwa chaguo la juu kwa asilimia 28, na huduma za afya kuchukua nafasi ya pili kwa asilimia 22. Ingawa asilimia 77 ya wahojiwa waliunga mkono uchaguzi wa shule, zaidi ya asilimia 60 walipinga kupatia nafasi kubwa kwa shule za binafsi katika mfumo wa elimu wa kitaifa.

Uchambuzi wa data ya moduli maalum ya Programu ya Utafiti wa Kimataifa wa Kijamii 2016 (ISSP) juu ya jukumu la serikali, ulioagizwa kwa ajili ya ripoti hii, ulishughulikia msaada wa elimu ya umma kwa kutumia sampuli ya nchi 35, zikiwemo nchi 10 za kipato cha kati. Kwa jumla, asilimia 89 ya watu wazima waliohojiwa walisema jukumu la msingi la kutoa elimu ya shule lilibaki kwa serikali, huku asilimia 6 wakisema familia na asilimia 5 ikasema taasisi nyingine (makampuni binafsi na mashirika ya faida; mashirika yasiyo ya faida, mashirika ya misaada na vyama vya ushirika; na mashirika ya kidini). Lakini, wahojiwa nchini India (asilimia 46), Ufilipino (asilimia 63) na Chile (asilimia 76) ndio waliokuwa katika kiwango cha chini cha kuunga mkono elimu kutolewa na serikali, ishara ya hali kubwa ya kupata elimu kutoka kwa washirika wengine ambao sio serikali **(Mchoro wa 1).**

HOJA TOFAUTI HUENDESHA MJADALA WA KUUNGA MKONO AU KUPINGA UTOAJI WA ELIMU USIO WA SERIKALI

Watetezi na wapinzani wa wahusika wasio wa serikali katika elimu huendeleza hoja zao kuhusiana na uwezo na uhalali wa wahusika wa serikali na wasio wa serikali katika kukuza ufanisi, uvumbuzi, usawa na ushirikishwaji katika elimu. Masuala haya hutazamwa kupitia lenzi ya ikiwa watu wanaamini elimu ni bidhaa au huduma ya kununuliwa kupitia soko na ikiwa watu wanapaswa kuwa na nafasi ya kuchagua elimu.


Je, gharama ya wahusika wasio wa serikali katika elimu ni nafuu? Watetezi wa shughuli zisizo za serikali katika elimu wanasema kuwa haziwezi kuepukika kwani serikali haiwezi kushughulikia mahitaji kamili ya elimu. Bila kujali kama wahusika wasio wa serikali wanachochewa na uhisani, imani na mawazo, au faida, ikiwa usambazaji wa bidhaa na huduma za elimu unakidhi mahitaji, basi soko linawezekana – ikiwa sio soko la kawaida, basi angalau lililopangwa. Kupitia soko, malengo ya gharama nafuu yanaweza kufuatiliwa.

1 Toleo la kikanda la ripoti hii juu ya wahusika wasio wa serikali katika elimu litatolewa kwa Asia Kusini.

MCHORO WA 1:

Katika nchi nyingi zilizoshiriki utafiti, zaidi ya asilimia 80 wanaunga mkono elimu kutolewa na serikali

Asilimia ya watu wazima waliosema kuwa jukumu msingi la kutoa elimu ni la serikali, 2016



GEM StatLink: https://bit.ly/GEM2021_Summary_fig1

Chanzo: Edlund na Lindh (2021) kulingana na 2016 ISSP.

Wapinzani wa shughuli zisizo za serikali katika elimu wanasema kuwa, ikiwa mazoea ya gharama nafuu yapo, yanapaswa kusambazwa katika mfumo wote wa elimu na kufanywa na shule zote, za serikali na zisizo za serikali. Ikiwa kutazuka mjadala kuwa walimu katika nchi wanalipwa pesa nyingi, basi hili linapaswa kuwa suala la kutatuliwa na sera ya umma, wala sio sababu ya kubadilisha muundo wa utoaji elimu. Wahusika wasio wa serikali wanaweza kupunguza gharama kwa kuajiri walimu vijana au wasiohitimu, ambalo sio suluhisho la kudumu. Kufanya ulinganisho wa kuaminika wa gharama kati ya shule za serikali na zisizo za serikali ni changamoto. Shule za umma mara nyingi huwahudumia watu zaidi wasiojiweza, ambao gharama ya kuwaelimisha huwa juu.

Je, wahusika wasio wa serikali hutoa usawa na ujumuishaji katika elimu? Watetezi wa utoaji wa elimu usio wa serikali wanasema kuwa watoa huduma wasio wa serikali husaidia kutimiza haki ya kupata elimu. Katika mazingira mengi, wahusika wasio wa serikali wamejaza mapengo ya kweli katika utoaji wa elimu, mara nyingi kwa vikundi visivyojiweza vilivyosahaulika na mifumo ya umma. Mara

nyingi serikali husita kuanzisha shule katika makazi yasiyo rasmi, kama ilivyo nchini Pakistani. Wahusika wasio wa serikali pia hutoa michango muhimu katika mazingira ya majanga na dharura, kama vile baada ya janga la tetemeko la ardhi la Nepal la 2015. Huko El Salvador, katika maeneo ya mijini yaliyokumbwa na vurugu na magenge, idadi ya waliojiandikisha katika shule zisizo za serikali ni mara mbili ile ya wastani wa kitaifa.

Wale wanaopinga shule zisizo za serikali wanaelezea shida zinazosababishwa na uchaguzi wa shule. Ikiwa wazazi wanaweza kuchagua shule wanayotaka, bila kanuni za kuwaongoza, basi walio matajiri zaidi wanaweza kumudu shule bora, mara nyingi zisizo za serikali, na kuzidisha ukosefu wa usawa, utabakishaji na ubaguzi. Uamuzi wa wazazi unahitaji maelezo mazuri, lakini maelezo juu ya sifa za shule hayapo au, ikiwa yapo, hutolewa bila usawa, na watu wengi wasiojiweza wana uwezo mdogo wa kuzifikia. Aidha, kuna watu kadhaa ambao ni vigumu kuwafikia ambao watoa huduma wanaweza kusita kuwapa huduma.

Baadhi ya wale wenye maoni kuwa serikali haipaswi kuwa na jukumu la msingi katika utoaji wa elimu wanapinga mamlaka yake kuamua juu ya maudhui ya elimu au uwezo wake wa kutoa elimu ya kiwango kinachohitajika. Wazazi wanaweza kutetea utoaji wa elimu wa kando na usio wa serikali, kutokana na wasiwasi kwamba shule ya umma ya karibu inatishia maadili ya jamii ya kitamaduni, kikabila, lugha au dini ambamo wanataka kumlelea mtoto wao. Lakini serikali zinaweza kusema kuwa suala hili linakinzana na ahadi yao ya kuhakikisha elimu yenye usawa na jumuishi na linaingilia uwezo wao wa kutekeleza viwango sawa katika juhudi za kutoa ubora sawa wa elimu kwa watoto wote, bila ubaguzi.

Je, wahusika wasio wa serikali huleta uvumbuzi zaidi kwenye elimu? Watetezi wa wahusika wasio wa serikali katika elimu wanasema kuwa inasaidia kuongeza uvumbuzi. Mawazo mengi ambayo yamebadilisha uelewa wa ufundishaji yaliibuka pembezoni mwa mifumo ya elimu ya umma au hata nje yake. Mifumo ya elimu ya umma imekuwa ofisi kubwa, rasimu, za pamoja za serikali ambazo zinaweza kusahau watu zinaofaa kuhudumia. Ukosoaji wa kawaida ni kwamba wanadhoofisha uchukuaji hatua, wanalazimisha usawazishaji na wanawafedhehesha wanafunzi na walimu.

Kufikia uvumbuzi ni kazi ngumu kwa mifumo ya elimu ya umma. Mabadiliko yanahitaji kupimwa na kujaribiwa ili kupima kama yanaweza kupanuliwa. Changamoto zinaweza kujumuisha vikwazo vya urasimu, upungufu wa uwezo kishirika, walimu na wazazi kutokuwa na motisha, uwezo finyu wa kifedha na kuingiliwa na kupingwa kisiasa. Hata hivyo, mifumo ya elimu ya umma haijaelekezwa vibaya katika suala la uvumbuzi kimakusudi. Na baadhi ya wahusika wasio wa serikali wanapima kama uvumbuzi fulani unafanya kazi katika elimu ya umma.


Mjadala juu ya uvumbuzi mara nyingi huvurugwa na dhana muhimu zinazotajwa kwa njia zinazopingana. Usawazishaji unakashifiwa na wale wanaopinga kile wanachokiona kama ugumu, utiifu na ukosefu wa kutofautisha wa mifumo ya elimu ya umma, lakini unatetewa na wale ambao wanapigania mitaala ya msingi ya kawaida ili kuhakikisha viwango vinafikiwa katika shule zote na ambao wanapendekeza kuwa ni shinikizo la ushindani, ambalo mara nyingi huchangiwa na watoa huduma binafsi, ambalo huharakisha utiifu. Mwishowe, suala la ikiwa usawazishaji unakatisha uvumbuzi linategemea ni viwango vipi vilivyobainishwa. Masharti kama vile 'uwajibikaji', 'uhuru' na 'uchaguzi' yamesifiwa na kukashifiwa kama kanuni za elimu za shirika. Ingawa lolote kati ya mawazo haya linaweza kuchunguzwa sifa zake, haimaanishi kuwa yanahalalisha jukumu kubwa kwa mashirika yasiyo ya serikali, na hasa ya binafsi, katika utoaji wa elimu.

VISASILI KUHUSU WAHUSIKA WA SERIKALI NA WASIO WA SERIKALI KATIKA ELIMU HUTAWALA

Visasili kumi vinavyojirudia kuhusu wahusika wa serikali na wasio wa serikali katika elimu vinadadisiwa katika ripoti hii yote.


KISASILI CHA 1.

Wahusika wa serikali na wasio wa serikali wanaweza kutofautishwa kwa njia bayana



Majadiliano ya wahusika wasio wa serikali katika elimu kawaida huhusisha uainishaji wa aina mbili: shule za umma na za binafsi. Katika hali halisi, mazingira ni changamano zaidi na tofauti si bayana vile. Wahusika wasio wa serikali wana tofauti nyingi. Huwa wanaingia katika sekta ya elimu kwa sababu tofauti zinazohusiana na mawazo, maadili, imani na maslahi. Wengi huingia katika mipango rasmi au isiyo rasmi na serikali, ikiwa ni pamoja na kandarasi na ushirikiano wa umma na wa kibinafsi, ambao hufanya iwe ngumu kutofautisha.

KISASILI CHA 2.
Kiwango cha ubinafsishaji kinajulikana.




Maelezo ya mienendo katika jukumu la wahusika wasio wa serikali mara nyingi hutegemea idadi ya taasisi binafsi katika jumla ya uandikishaji. Je, nchi zinawachukuliaje walimu wa shule za umma wanaoongeza mapato yao kwa kuwafundisha wanafunzi baada ya saa za kazi? Je, ni kwa kiasi gani mfumo wa elimu ambao hupeana kandarasi za vitabu vya kiada, tathmini au usimamizi wa data, au hata upishi na usafirishaji, unaweza kusemekana kuwa wa umma? Je, sera ya serikali iliyoandikwa na mtetezi wa haki bado inachukuliwa kuwa ya umma?

KISASILI CHA 3.
Sekta binafsi ndiyo ya kulaumiwa kwa ubinafsishaji katika elimu.



Idadi kubwa ya watoa huduma binafsi ni shule za mmiliki mmoja. Walijitokeza baada ya wazazi kuonyesha wasiwasi wa kweli kuhusu ubora wa shule za umma uliozoroteshwa na upuuzaji. Wakati kuzorota kwa ubora kulikuwa wazi, familia tajiri na kwa kiwango kidogo masikini ziliondoka kwenye mfumo wa umma, hatua iliyopunguza uungwaji mkono wa mfumo huo na kuuacha ukiwa hauna fedha za kutosha. Kuamini matabaka miongoni mwa viongozi wa kisiasa kuliwafanya wavumilie zaidi ukosefu wa usawa na kupunguza kujitolea kwao kulinda elimu ya umma na watu wasiojiweza ambao walinufaishwa na elimu hiyo.


KISASILI CHA 4.
Elimu ya umma ina usawa.



Kaya mara nyingi hupata gharama kubwa za elimu kupitia ada zilizofichwa, malipo wanayogharamia yanayoweza kuepukwa na matumizi ya ziada ili kufidia kile ambacho shule za umma hazitoi. Ingawa ni kawaida kukosoa mifumo ya elimu ambayo imefungua milango kwa watoa huduma wasio wa serikali, jambo linalozidisha ukosefu wa usawa, mifumo mingi ya elimu ya umma inashindwa kuzuia utabakishaji na ubaguzi.

KISASILI CHA 5.

Wazazi huchagua shule kwa misingi ya maelezo thabiti kuhusu ubora.



Dhana ya msingi miongoni mwa wanaounga mkono shule zisizo za serikali na uchaguzi wa shule ni kwamba wazazi, kama wateja, wanapata habari kuhusu shule bora na wanatumia habari hizo kwa ufanisi. Katika hali halisi, data juu ya athari za shule ni changamano sana kwa nchi nyingi kuidhibiti na kuiwasilisha. Na mara nyingi wazazi hupuuza habari kama hizo, na kuchagua shule zinazowavutia kwa sababu nyinginezo: imani za kidini, urahisi wa kufikia na sifa za kidemografia za wanafunzi.

KISASILI CHA 6.

Ushindani hufanya shule kuwa bora.



Uwajibikaji na ushindani mzuri huchochea baadhi ya watu kuwa bora. Katika nyanja za kiuchumi, makampuni hushindana ili kuwepo, kwani sababu yao ya kuwepo ni kupata faida. Lakini si bayana athari za mienendo kama hiyo katika elimu. Tafiti zinazoonyesha athari za ushindani katika mfumo mzima ni nadra, kwani mada yenyewe ni changamano, na matokeo hayajahitimishwa. Isitoshe, ushindani unaweza kusababisha shule zisizo za serikali kujizatiti kutimiza matarajio ya wazazi, kinyume na mazoezi mazuri ya ufundishaji.

KISASILI CHA 7.


Shule na vyuo vikuu vya binafsi ni bora.



Ulinganisho wa viwango vya shule za umma na za binafsi vya kufaulu katika mitihani ndio ushahidi wa kawaida unaotegemewa ili kuorodhesha shule kama inavyoripotiwa na vyombo vya habari na kusomwa na wazazi. Katika hali halisi, usajili wa wanafunzi unatofautiana, huku wazazi wenye uwezo wa kifedha, elimu bora na wenye matarajio makubwa wakiwa na uwezekano mkubwa wa kuchagua shule ya binafsi. Shule binafsi, kwa upande wake, zinaweza kuwachuja wanafunzi ili kuongeza uwezekano wa matokeo ya juu. Sababu hizo zinapodhibitiwa, pengo kati ya shule za umma na za binafsi kwa kawaida hupungua au kufutwa.

KISASILI CHA 8.


Sekta binafsi ni suluhisho la changamoto ya kutokuwa shuleni



Huku zaidi ya wanafunzi milioni 350 wa shule za msingi na sekondari wakiwa katika taasisi za binafsi, kunaweza kuwa na mgogoro ikiwa wanafunzi hawa watabadili na kujiunga na mfumo wa elimu wa umma. Hata hivyo, shule za binafsi zimeshamiri katika maeneo ya mijini, ambapo tayari karibu kila mmoja amejiunga na shule. Kwa kiasi kikubwa, shule hizi hazipo vijijini. Na katika nchi za kipato cha chini na cha kati, watoto kutoka asilimia 20 ya familia tajiri zaidi wana uwezekano mara 10 zaidi wa kuhudhuria shule ya binafsi ikilinganishwa na wenzao kutoka asilimia 20 ya familia masikini zaidi.

KISASILI CHA 9.

Sekta binafsi ni suluhisho la upungufu wa fedha za elimu.



Mara nyingi huwa kuna matumaini makubwa kwamba sekta binafsi inaweza kuchukua jukumu muhimu katika kufadhili elimu ili kusaidia kufikia Lengo la 4 la Maendeleo Endelevu. Hakuna ushahidi kufikia sasa kwamba sekta hiyo iko tayari au ina uwezo wa kufanya hivyo. Lakini inaweza kuchangia kwa njia zingine, kwa mfano kupitia kodi, hasa katika nchi za kipato cha chini na cha kati ambapo viwango vya ukusanyaji wa mapato ya ndani viko chini na fursa za kuepuka na kukwepa kulipa kodi ni nyingi. Sekta binafsi inaweza kuongoza zaidi katika kukuza ujuzi na kutoa huduma za utunzaji wa watoto kulingana na kanuni za kitaifa.

KISASILI CHA 10.

Kanuni zinaweza kushughulikia wasiwasi wote kuhusu utoaji wa elimu usio wa serikali.



Kuna makubaliano kwamba shughuli zisizo za serikali katika elimu zinapaswa kudhibitiwa. Lakini kanuni hazishughulikii kikamilifu jinsi ya kuendeleza usawa na ubora katika mfumo mzima. Ni serikali chache zinazofuatilia ikiwa kuhamia kwa kaya tajiri kwenda shule za binafsi kunagawanya mfumo wa elimu au jinsi matumizi ya kaya kugharamia elimu yanavyoongeza ukosefu wa usawa. Serikali nyingi huruhusu uandikishaji wa shule wenye ubaguzi. Ni serikali chache zinazodhibiti utetezi au masomo ya ziada ya binafsi, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limesalia bila kufafanuliwa na kusingizia ushirika. Ni serikali chache zaidi zenye rasilimali za kutiisha na kutekeleza kanuni kwa ufanisi.

Karibu miaka 25 iliyopita nchini Marekani, wakati ushahidi ulipoanza kujitokeza kuhusu athari zisizo na usawa za aina mpya ya elimu ya umma ya kitaasisi iliyojikita kwenye uchaguzi wa shule, waandishi wa utafiti wa mapema walifupisha matokeo kwa maswali mawili: Ni nani anayechagua? Ni nani anayepoteza? (Fuller na Elmore, 1996). Kadri ushahidi zaidi unavyoendelea kukusanyika kuhusu mbinu, ufanisi na matokeo ya uchaguzi wa shule kote ulimwenguni, Ripoti ya Ufuatiliaji wa Elimu Ulimwenguni inapeleka maswali haya kwa hadhira ya ulimwengu. Vipengele vinne muhimu vya shughuli zisizo za serikali – utoaji, udhibiti, ufadhili na ushawishi - vinashughulikiwa katika elimu ya msingi na ya sekondari, ikifuatiwa na kuangalia kwa kina zaidi mambo haya katika viwango vingine vya elimu, ambavyo huwa havizingatiwi sana: elimu ya chekechea, elimu ya juu, ya ufundi na ya watu wazima.

UTOAJI WA ELIMU

Uandikishaji wa wanafunzi katika shule zisizo za serikali umekuwa ukiongezeka. Idadi ya taasisi binafsi duniani kote iliongezeka kwa asilimia 7 katika kipindi cha miaka 10, kutoka asilimia 10 mwaka wa 2002 hadi asilimia 17 mwaka wa 2013 katika elimu ya msingi, na kutoka asilimia 19 mwaka wa 2004 hadi asilimia 26 mwaka wa 2014 katika elimu ya sekondari, lakini tangu wakati huo imebaki pale **(Mchoro wa 2).**


Umiliki, usimamizi na ufadhili ndivyo vigezo vya kawaida vya kufafanua sekta isiyo ya serikali. Uhusiano wa watoa huduma na serikali, kinachowachochea na bei zao zinaweza kutumiwa kuwaweka katika vikundi. Uchambuzi wa ripoti hii uligundua kuwa shule za kidini zinaweza kupatikana katika nchi 124 kati ya 196. Shule za mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) na zile za jamii zinaweza kupatikana katika nchi 74 kati ya 196, mara nyingi katika mazingira ya dharura. Shule za faida ni chache, isipokuwa katika miktadha michache, kama vile Falme za Kiarabu. Aina pana ya shule za bei ya wastani, nyingi zikiwa zinamilikiwa na mtu mmoja katika nchi za kipato cha chini na cha kati katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Asia zinajulikana kama shule za binafsi za ada ya chini.

Shule za serikali na zisizo za serikali hutofautiana katika usajili wa wanafunzi na rasilimali. Ni watoto wachache maskini wenye chaguo la kuhudhuria shule za binafsi. Kutathmini ubora wa elimu, wazazi hurejelea ukubwa wa darasa, ubora na juhudi za walimu, kasi ya shule ya kuchukua hatua, nidhamu na usalama, lugha ya kufundishia, dini, kabila na utamaduni. Nchini Uingereza, uchambuzi wa shule 18,000 za Kiingereza ukilinganisha shule za umma na zile za umma zilizobinafsishwa ulitambua asilimia kubwa ya walimu wasiohitimu katika aina ya pili ya shule. Shule za umma na za binafsi zinaweza kutofautiana katika rasilimali zingine. Katika Amerika ya Kusini, idadi wastani ya kompyuta kwa kila mwanafunzi katika shule binafsi ni maradufu ile ya shule za umma.

MCHORO WA 2:

Viwango vya kujiandikisha katika shule binafsi viko juu zaidi katika eneo la Kusini mwa Asia

Viwango vya kujiandikisha katika taasisi binafsi, kulingana na viwango vya elimu, 1990–2019



GEM StatLink: https://bit.ly/GEM2021_Summary_fig2

Chanzo: Hifadhidata ya UIS.

Ushahidi mwingi unaonyesha kuwa faida ya kimasomo ya kwenda katika shule za binafsi ni finyu. Takwimu za nchi 31 za kipato cha chini na cha kati zilionyesha kuwa makadirio ya thamani kutokana na kuhudhuria shule za binafsi yalishuka kwa nusu hadi theluthi mbili baada ya kurekebisha utajiri wa kaya. Aidha, ingawa utoaji wa elimu ya msingi usio wa serikali unaweza kujaza mapengo kwa muda mfupi au wa kati, unaweza kusababisha ubaguzi na ukosefu wa usawa. Nchini Uswidi, manispaa 29 kati ya 30 zilikuwa na shule za sekondari za vidato vya chini zilizokuwa na kiasi kikubwa cha ubaguzi; katika manispaa 16, ubaguzi ulionekana kwa kiasi kikubwa kusababishwa na uchaguzi wa shule. Ingawa ushindani na shule zisizo za serikali unatarajiwa kuchochea shule za umma kuimarika, uwepo pekee wa shule za binafsi au zingine katika maeneo ya karibu hauweza kuwa hamasisho la kutosha kwa mamlaka ya shule za umma kuchukua hatua ikiwa hazina rasilimali za kifedha au uhuru wa kuchukua hatua.

Masomo ya ziada ya binafsi yako karibu kila mahali. Dhana hii, ambayo imeenea katika nchi kadhaa za Asia Mashariki na Nchi za Kiarabu, pia inaenea katika maeneo ambapo haikuwepo, kama vile Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na kaskazini mwa Ulaya. Mahitaji ya masomo ya ziada mara nyingi huhusishwa na haja ya wanafunzi kujiandaa kwa ajili ya mitihani muhimu ili kuwaongezea nafasi ya kufaulu. Lakini athari za ukufunzi kwa matokeo ya wanafunzi binafsi ni mseto: Baadhi ya tafiti zimegundua athari chanya kwa wale walio nyuma zaidi, huku tafiti zingine zikionyesha kwamba ukufunzi hauna athari chanya zenye utaratibu kwenye matokeo ya wanafunzi. Aidha, ukufunzi unaweza kudhoofisha utendaji wa mfumo wa elimu kwa kuathiri vibaya tabia ya wanafunzi na walimu.

Sera ya vitabu vya kiada, ununuzi na usambazaji hutofautiana kulingana na kiwango cha serikali cha kuhusika. Katika baadhi ya nchi, uchapishaji kimsingi hufanywa na makampuni yanayomilikiwa na kudhibitiwa na serikali; katika nchi nyingine, kuna mfumo mseto wa uchapishaji wa umma na wa binafsi. Nchi kadhaa za mapato ya juu, ikiwemo Uhispania, sana sana huacha uchapishaji wa vitabu vya kiada kwa watoa huduma wa kibiashara, na serikali inahusika katika kutoa mwongozo na kuidhinisha mapendekezo. Maingiliano kati ya wachapishaji wa kimataifa, wafadhili na maslahi ya ndani mara nyingi huathiri mabadiliko ya kufanyia uchapishaji ndani mwa nchi katika nchi maskini. Kwa mfano, tasnia ya vitabu vya kiada nchini Gabon inaongozwa na Edicef, kampuni ya kuchapisha vitabu inayomilikiwa na Hachette Livre ya Ufaransa, mmoja wa wachapishaji wakubwa zaidi duniani.

Shinikizo la kutayarisha maudhui dijitali linaongozwa na makampuni makubwa ya uchapishaji na ya teknolojia. Pearson, kampuni inayoongoza katika soko la kimataifa la kuchapisha maudhui ya elimu, ilibadilisha kauli mbiu yake kutoka 'mchapishaji mkubwa duniani wa vitabu vya kiada na vifaa vya kufundishia mtandaoni' (world's largest publisher of textbooks and online teaching materials) hadi 'kampuni ya ulimwengu ya mafunzo kidijitali' (world's digital learning company), na kuzingatia zaidi masomo na tathmini za mtandaoni. Zaidi ya wachapishaji wa vitabu vya kiada wa kimataifa na kikanda, vigogo wa teknolojia wameingia katika sekta ya elimu ya mtandaoni, mwelekeo ulioimarishwa wakati wa janga la COVID-19. Uchambuzi wa uzoefu wa mchakato wa ununuzi wa teknolojia ya elimu nchini Marekani uligundua kuwa shule na wilaya za shule zilikuwa zimezidiwa na maelfu ya wachuuzi wa teknolojia ya elimu wanaouza aina nyingi za bidhaa.

Serikali zinatoa kandarasi zaidi za huduma za ziada katika elimu. Wakosoaji wa utoaji kandarasi wanahofia kuwa ubinafsishaji unaweza kudhoofisha huduma za umma na utaalamu. Uchambuzi wa Australia uligundua kuwa kuwapa kandarasi wafanyakazi zaidi wa kusafisha kulisababisha kuongezeka kwa wanakandarasi, kuongezeka kwa visa vya malipo duni, kupungua kwa saa za kusafisha na viwango vya chini vya afya na usalama kazini.

USIMAMIZI NA UDHIBITI

Usimamizi wa watoa huduma za elimu wasio wa serikali mara nyingi huwa umegawanyika. Usimamizi bora na udhibiti unaofaa ni vigezo muhimu vya uwezo wa serikali kutoa elimu bora yenye usawa. Katika nchi 94, mipango au mikakati ya sekta inataamali wahusika wasio wa serikali wakishiriki katika utoaji wa elimu au wa huduma nyingine. Wizara au idara zinashirikiana majukumu katika baadhi ya nchi. Mgawanyiko, ukosefu wa uratibu na kuingiliana au ufafanuzi usio bayana wa majukumu unaweza kuathiri vibaya usawa na ubora. Wizara za elimu zinasimamia watoa huduma wasio wa serikali katika asilimia 83 ya nchi, huku asilimia 13 ya nchi zikiwa na mamlaka nyingi. Ni asilimia 39 tu ya nchi zilizo na idara, kitengo au wakala wa elimu ya binafsi katika ngazi ya kitaifa chini ya wizara ya elimu. Wizara za masuala ya kidini, badala ya wizara za elimu, zinasimamia shule za kidini katika asilimia 22 ya nchi – na asilimia 70 katika Afrika ya Kaskazini na Asia ya Magharibi.

Njia za ufadhili zinaathiri usimamizi. Wahusika wasio wa serikali hupata msaada wa moja kwa moja au usio wa moja kwa moja wa kifedha wa serikali wa aina mbalimbali:

misaada kwa wanafunzi (katika asilimia 79 ya nchi), ruzuku kwa wazazi (asilimia 19), msaada wa mishahara ya walimu au sehemu zingine za uendeshaji (karibu asilimia 60) na mikopo au zawadi (asilimia 19). Ubia wa umma na wa kibinafsi unahusisha viwango anuwai vya ushiriki kati ya kila mhusika na mipango anuwai ya sera na udhibiti. Ukaguzi wa tafiti juu ya mifumo ya ufadhili uligundua kuwa mara nyingi athari zilikuwa hasi. Katika angalau theluthi mbili ya tafiti 98, athari kwa usawa wa ruzuku, mipango ya vocha na mipango ya mkataba zilionekana kuwa hasi.

Kanuni zinapaswa kusaidia kuimarisha ubora na usawa katika elimu. Karibu nchi zote zina kanuni zinazoelezea mahitaji ya kuingia na kuendesha shule zisizo za serikali, pamoja na usajili na upataji leseni. Katika asilimia 80 ya nchi, kuna kanuni juu ya mahitaji ya nafasi, kama vile ukubwa wa jengo au kipande cha ardhi na kipimo cha chini cha nafasi ya darasa. Katika jimbo la Haryana nchini India, majengo yanahitaji kumilikiwa au kukodiwa kwa angalau miaka 20 ili kuanzisha shule. Jimbo jingine, Uttar Pradesh, hutumia vigezo viwili vya kutambua shule: kiwango cha chini cha eneo kwa kila mwanafunzi (mita 9 za mraba) na ukubwa wa darasa (mita 180 za mraba). Sheria pia zinagusia masuala ya maji na usafi wa mazingira. Katika asilimia 47 ya nchi zilizo na data, vyoo vya jinsia moja vinahitajika katika shule zisizo za serikali. Katika asilimia 74 ya nchi, uwiano wa wanafunzi na walimu hudhibitiwa. Karibu asilimia 45 ya nchi zina kanuni kuhusu taratibu za uandikishaji katika shule zisizo za serikali, huku asilimia 67 zikidhibiti ada za shule zisizo za serikali katika elimu ya lazima. Zaidi ya nusu wana kanuni juu ya mtaala. Katika kipindi cha miaka 10, nchi 21 zimezindua kanuni juu ya kutengeneza faida na 80 juu ya utoaji vyeti kwa walimu.

Utekelezaji dhaifu na uwajibikaji usioridhisha vinadhoofisha ubora wa elimu na usawa. Kuweka kanuni hakumaanishi kuwa watoa huduma wasio wa serikali wanazizingatia. Katika baadhi ya nchi za kipato cha chini na cha kati, taratibu changamano, ghali au ndefu za usajili huwazuia watoa huduma kupata utambulisho rasmi. Serikali ya jimbo la Lagos nchini Nigeria ilikuwa imeidhinisha shule 1 tu kati ya 4 miongoni mwa shule 20,000 za binafsi kufikia mwaka wa 2021. Takwimu za angalau nchi 27 zinatambua shule ambazo hazijasajiliwa. Uganda inaainisha shule zisizo za serikali katika makundi ya zenye leseni, zilizosajiliwa na zisizosajiliwa: asilimia 14 ya shule za msingi na asilimia 13 ya shule za sekondari hazijasajiliwa. Kutokuwa na usimamizi kunaweza kusababisha uteuzi wa wanafunzi usio rasmi. Katika Bogotá, Kolombia, mpango wa Shule Maalum (Concession School) wa shule za mkataba, ulioanzishwa ili kuwahudumia wanafunzi walio katika mazingira magumu, ulikuwa na sera ya uandikishaji iliyozingatia kutobagua na umbali wa makazi; katika hali halisi, ingawa haikufanywa rasmi, wanafunzi walichaguliwa kwa misingi ya matokeo ya kimasomo.

Michakato na viwango vya kuhakikisha ubora vinatofautiana. Kimsingi kila nchi hutekeleza viwango vya shule zisizo za serikali kupitia ukaguzi wa shule. Katika asilimia 81 ya nchi, wajibu huu unahusu aina zote za shule zisizo za serikali; katika asilimia 6, unahusu shule zinazosaidiwa na serikali tu. Aidha, asilimia 81 ya nchi zina kanuni zinazoamuru ushiriki wa shule zisizo za serikali katika tathmini pana. Katika zaidi ya nusu ya nchi hizo, wajibu huo unahusu aina zote za shule zisizo za serikali, huku katika asilimia 12, unahusu tu shule zinazosaidiwa na serikali.

Njia zinazofaa za uwajibikaji, vikwazo na njia za kurekebisha pia zinaweza kuhimiza utiifu. Serikali inapaswa kuwawajibisha watoa elimu kufuata viwango vya ubora, uchukuaji hatua, usalama na ujumuishaji. Karibu nchi zote zinatumia vikwazo, kufungwa kwa shule au kuondolewa kwa leseni ikiwa shule zisizo za serikali hazizingatii kanuni. Asilimia 54 ya nchi pia hudhibiti muda wa vipindi hivyo vya kufungwa. Takriban nchi 90 zina kanuni za maadili au usimamizi kwa ajili ya walimu na wafanyakazi wa shule, ambazo mara nyingi huwajumuisha watoa huduma wasio wa serikali.

Ukufunzi wa ziada wa binafsi mara nyingi haudhibitiwi. Ukufunzi wa binafsi haudhibitiwi katika asilimia 48 ya nchi. Nchi 53 tu ndizo zinazoudhibiti katika sheria ya elimu, huku 19 zikiwa zinaudhibiti chini ya sheria ya kibiashara. Katika asilimia 31 ya nchi, kanuni zinabainisha sifa zinazohitajika za wakufunzi; nchi 10 zinapiga marufuku wazi ukufunzi. Nchini Uchina, sheria ya mwaka 2021 inapiga marufuku kampuni zinazofundisha mitaala ya lazima ya masomo kupata faida na pia kutafuta mtaji, hivyo kuzuia kutolewa kwa leseni mpya. Makampuni yanahitaji kuwa mashirika yasiyo ya faida ili kuendelea na shughuli. Serikali imeanzisha idara maalum kwa ajili ya kusimamia na kufuatilia makampuni binafsi ya ukufunzi.

FEDHA

Serikali hutofautiana katika maamuzi yao kuhusu ikiwa na jinsi ya kufadhili watoa huduma wasio wa serikali. Nchini Kanada, serikali inalipia asilimia 30 ya matumizi ya shule za binafsi lakini asilimia 94 ya matumizi ya shule za umma. Nchini Uholanzi, shule zote, bila kujali aina, hupokea ruzuku kubwa ya gharama ya wafanyakazi na shughuli za uendeshaji na fedha za ziada kwa wanafunzi kutoka jamii zisizojiweza kiuchumi ambao wana mahitaji maalum ya elimu. Tangu 2000, nchi kadhaa, zikiwemo Chile, Hungaria,

Uswidi na Uingereza, zimepata ongezeko la shule za binafsi tegemezi zinazojiandikisha, zile zinazopokea angalau asilimia 50 ya fedha zao kutoka kwa serikali.

Serikali hugharamia tu baadhi ya matumizi ya shule zisizo za serikali. Nchini Bangladesh, zaidi ya shule 16,000 za sekondari zisizo za serikali na madrasa 7,600, ambazo kwa pamoja huandikisha asilimia 96 ya wanafunzi wote, hupokea malipo ya kila mwezi kwa ajili ya mishahara ya walimu. Lakini Haiti, ambapo asilimia 85 ya shule za msingi si za serikali, haisimamii gharama za mishahara. Nchini India, ni asilimia 6 pekee ya shule za msingi na sekondari zilizopokea ruzuku kwa ajili ya mishahara ya walimu mnamo 2019/20. Nchini Indonesia, madrasa na shule za bweni za Kiislamu, zinazojulikana kama pesantren, ambazo ni asilimia 35 ya shule zote za binafsi, hazijumuishwi kwenye baadhi ya njia za ufadhili.

Baadhi ya serikali zinaunga mkono uandikishaji wa wanafunzi wasiojiweza katika shule zisizo za serikali. Nchini India, Sheria ya Haki ya Elimu ya 2009 ilizitaka shule za binafsi kutoa asilimia 25 ya nafasi za darasa la 1 kwa watoto kutoka familia zenye kipato cha chini; nayo serikali kwa upande wake ikazifidia gharama yao ya masomo. Kwa upande mwingine, Côte d 'Ivoire, ambapo idadi ya wanafunzi katika shule za sekondari za ruzuku iliongezeka mara nne kati ya 2010/11 na 2017/18, haikuzingatia upatikanaji wenye usawa.

Kaya hukabiliwa na mzigo mkubwa na machaguo magumu. Kama sehemu ya Pato la Taifa, matumizi ya elimu ya kaya yanafikia asilimia 0.3 katika nchi za kipato cha juu na asilimia 1 katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Matumizi haya ni asilimia 1.2 ya Pato la Taifa nchini El Salvador, asilimia 1.5 nchini Moroko, asilimia 1.8 nchini India na asilimia 2.5 nchini Ghana. Wakati asilimia 20 ya kaya masikini hazitumii chochote kwa elimu nchini Argentina, Kostarika, Ufilipino na Zambia, asilimia 20 ya matajiri hutumia kati ya asilimia 0.5 na asilimia 1.7 ya Pato la Taifa.

Elimu ya umma si ya bure. Karibu theluthi moja ya matumizi ya kaya katika nchi za kipato cha chini na cha kati hutoka kwa kaya zilizo na watoto katika shule za umma. Kaya zilizo na watoto katika shule za binafsi zinawakilisha asilimia 80 ya matumizi nchini Gwatemala na Pakistani; kaya zilizo na watoto katika shule za umma zinawakilisha asilimia 60 ya matumizi nchini Uchina na Kenya. Katika maeneo ya vijijini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zaidi ya robo tatu ya familia huona michango ya shule za msingi kama ya lazima, zikisema kuwa watoto wanaweza kuadhibiwa ikiwa michango itachelewa. Nchini Australia, michango ya wazazi inazidisha ukosefu wa usawa kati ya shule.

Ukufunzi wa ziada wa binafsi ni gharama kubwa kwa kaya nyingi. Nchini Uchina, kaya zilitenga karibu theluthi moja ya matumizi yao yote ya elimu kugharamia matumizi ya nje ya shule katika mwaka wa 2017. Kiasi hiki kilikuwa kati ya asilimia 17 katika kaya za vijijini hadi asilimia 42 katika kaya za mijini. Nchini Misri, kama sehemu ya wastani wa matumizi kwa kila mtu, miongoni mwa wanafunzi wa elimu ya sekondari, wale wa kaya tajiri zaidi walitumia asilimia 51 kwenye masomo ya binafsi na kaya maskini zikatumia asilimia 29. Nchini Myanmar, ukufunzi uliwakilisha asilimia 42 ya jumla ya matumizi ya elimu ya kaya.

Watoa huduma binafsi hutegemea matumizi yanayogharamiwa na kaya. Shule nyingi za sekondari za binafsi hupokea angalau asilimia 80 ya mapato yao kutoka kwa ada katika mifumo 28 kati ya 51 ya elimu ya nchi za kipato cha kati na cha juu. Katika nchi za kipato cha chini na cha chini kiasi, wazazi maskini hutumia mikakati mbalimbali ili kukabiliana na gharama za shule binafsi. Ulimwenguni, familia moja kati ya sita huweka akiba ili kulipa ada ya shule, huku karibu asilimia 8 ya kaya pia zikikopa. Huko Haiti, Kenya, Ufilipino na Uganda, asilimia 30 ya kaya au zaidi hukopa kwa ajili ya ada ya shule.

Ufadhili wa shule za binafsi umeathiriwa pakubwa na COVID-19. Janga hilo liliathiri shule za binafsi, hasa zile zinazotegemea ada ya shule. Nigeria ilizindua mfuko wa kuchochea wa mikopo ya riba nafuu kulipa walimu wa shule binafsi. Nchini Ghana, shule za binafsi zilipokea msaada kama sehemu ya mpango wa jumla wa biashara ndogo na za kati. Viet Nam ilipanua mipango ya uhawilishaji wa pesa ili kujumuisha walimu wa shule za binafsi. Nchini Panama, asilimia 35 hadi 40 ya wazazi hawakuweza kulipa ada ya kila mwezi. Nchini Ekwado, uandikishaji katika shule za umma uliongezeka kwa asilimia 6.5, au wanafunzi 120,000, ambao walihama kutoka shule za binafsi.

Matumizi ya fedha za misaada kwa ajili ya elimu binafsi hupingwa. Kutoka mfuko wa elimu wa karibu dola bilioni 1.2 za Marekani, Shirika la Fedha la Kimataifa lilipatia vikundi vya shule za binafsi asilimia 15 lakini likasimamisha uwekezaji wake katika shule za binafsi zinazotoza ada mnamo 2019, kufuatia shinikizo kutoka kwa mashirika ya kiraia. Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu ulianzisha mkakati wa sekta binafsi lakini upinzani wakati wa majadiliano ulisababisha kifungu kinachozuia matumizi ya fedha zake kusaidia utoaji wa huduma za msingi za elimu zinazozalisha faida.

Wafadhili wanafanyia majaribio ubia wa sekta ya umma na ya binafsi. Serikali zilizokosa fedha zimetafuta mtaji wa kibinafsi ili kuboresha na kupanua miundombinu ya elimu ya umma nchini Misri, Ufilipino na Afrika Kusini. Baadhi ya

wafadhili wameangalia suala la kutumia fedha zao kama kichocheo cha kuongeza fedha kupitia ushirika huo. Lakini kuna wasiwasi kwamba serikali ambazo zinaweza kubuni, kutekeleza na kudhibiti ubia zinafaa zaidi kutumia njia za umma kufikia malengo yao.

Mchango wa kifedha wa shughuli za uhisani na za mashirika katika elimu ni mdogo. Licha ya maoni kwamba kiasi ambacho mashirika ya uhisani yanatumia katika elimu kinaongezeka, bado kiasi hiki ni kidogo. Uchambuzi taratibu wa misaada ya uhisani kutoka mashirika 143 katika Mtandao wa Mashirika Yanayokuza Maendeleo (Network of Foundations Working for Development), mpango wa Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (OECD), unakisia kwamba elimu ilipokea dola bilioni 2.1 za Marekani katika kipindi cha miaka mitatu, kuanzia 2013 hadi 2015. Kiasi hiki kilikuwa asilimia 9 ya ufadhili wote wa uhisani.

USHAWISHI

Hoja kuhusu ufanisi, uvumbuzi na usawa ni sehemu msingi ya mijadala juu ya jukumu la wahusika wasio wa serikali katika elimu. Mijadala hii mara nyingi huwa imejawa na chuki na kutoaminiana wakati maoni mawili tofauti ya ulimwengu yanakinzana. Makundi mbalimbali ya wahusika hujaribu kushawishi maoni ya umma na sera ya elimu ili kuunga mkono au kupinga wahusika wasio wa serikali kupewa nafasi kubwa zaidi. Zana wanazotumia ni mitandao ya utetezi na ushawishi, utafiti na ufadhili, ambazo mara nyingi huhusishwa na mauzo ya bidhaa na huduma. Katika ushindani huu wa mawazo ya kisiasa na maslahi ya kiuchumi, ambapo wahusika hutumia njia halali na zisizo halali ili kufanya maoni yao kushinda, changamoto iliyopo ni kudumisha uwazi na uadilifu wa mchakato wa sera ya elimu ya umma na kuzuia maslahi binafsi.

Vikundi vingi husika havina msimamo sawa kuhusu watoa huduma wasio wa serikali katika elimu. Mashirika ya kiraia mara nyingi huwa muhimu, kwani huwa yanatoa maoni yao juu ya elimu kufanywa kama bidaa na kubinafsishwa. Wao husema kuwa elimu lazima ibaki chini ya udhibiti wa kidemokrasia. Lakini hata ndani ya harakati zinazozingatia haki, kama vile Kampeni ya Kimataifa ya Elimu, wanachama wanashikilia maoni yenye tofauti ndogondogo yanayoathiriwa na hali halisi katika nchi zao. Katika utafiti wa wanachama uliofanywa kwa ajili ya ripoti hii, asilimia 43 walipinga utoaji wa elimu unaolenga faida lakini asilimia 12 waliunga mkono; kuhusu ubia kati ya wadau wa umma na wa binafsi, waliounga mkono walikuwa asilimia 41 na waliopinga walikuwa asilimia 20. Wengine walikuwa na maoni mseto.

Mitandao ya utetezi ya kimataifa imesema ubinafsishaji na uchukuliaji wa elimu kama biashara ni vitisho kwa haki ya kupata elimu. Mtazamo huu umeelezwa katika Kanuni za Abidjan juu ya majukumu ya haki za binadamu ya Mataifa kutoa elimu kwa umma na kudhibiti ushiriki wa kibinafsi katika elimu. Mnamo 2018, raia 10 wa Kenya waliwasilisha malalamiko kwa Mchunguzi wa Mshauri wa Utekelezaji, ofisi huru ya uwajibikaji ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), wakidai kuwa Shule za Kimataifa za Bridge, zilizokuwa za faida, zilikuwa zinakiuka viwango vya mtaala, afya na usalama na kazi. Mnamo 2020, shirika la IFC lilisimamisha uwekezaji katika vikundi vya shule huku Kikundi Huru cha Tathmini cha Benki ya Dunia kikizindua tathmini ya uwekezaji katika shule za binafsi.

Msaada na rasilimali zinazotolewa na mashirika mengi ya kimataifa kwa watoa huduma wasio wa serikali bila kutathmini huathiri ajenda. Miongoni mwa njia ambazo Benki ya Dunia hushawishi utungaji wa sera ni moduli juu ya ushiriki wa sekta binafsi, inayochukuliwa kuwa moja ya maeneo 13 muhimu ya sera ya kuendeleza masomo chini ya Njia inayotumia Mifumo ili Kufikia Matokeo Bora ya Elimu. Moduli hii imependekeza upanuzi wa utoaji wa elimu ya binafsi katika nchi 9 kati ya 10. Mfuko wa Matokeo ya Elimu unaofadhiliwa na UNICEF huvutia wawekezaji wanaolenga athari katika miradi ya ufadhili inayolenga matokeo, ambayo haina rekodi nzuri ya matokeo katika elimu. Mashirika ambayo yamenufaika na msaada wa kimataifa ni pamoja na Ark, shirika ambalo limepanuka kutoka kuendesha shule za umma nchini Uingereza hadi kushauri na kusaidia kutekeleza ushirikiano wa wadau wa umma na wa binafsi katika nchi ikiwa ni pamoja na Liberia na Afrika Kusini.

Misimamo ya Mashirika juu ya jukumu ambalo yanadhani wahusika wasio wa serikali wanapaswa kutekeleza katika elimu hutofautiana. Mashirika ya makampuni na ya uhisani huwa na motisha zinazotofautiana hivyo ni vigumu kuyaainisha kama kundi. Mara nyingi, mashirika hukosolewa kwa kujaribu kushawishi sera kuelekea pande fulani. Shirika la kihisani la Lemann Foundation lilisaidia kuanzisha viwango vya kitaifa vya kujifunza nchini Brazil baada ya mashauriano kadhaa.

Miungano ya walimu imekuwa mstari wa mbele katika juhudi za utetezi za kuunga mkono elimu ya umma. Miungano hii imefichua kwa ufanisi majaribio ya kudhoofisha elimu ya umma kupitia utoaji wa kandarasi za huduma za umma na kuzifanya kuwa kama biashara bila sababu. Education International, shirikisho la miungano ya walimu, limekuwa likihoji kama matumizi makubwa ya ushirikiano wa wadau wa umma na wa binafsi katika Amerika ya Kusini, kwa mfano nchini Kostarika na Jamhuri

ya Dominika, yameathiri taasisi za umma zinazo shughulikia malengo sawa. Lakini katika baadhi ya matukio, mbinu za miungano hii zimekosolewa kwa kudhoofisha juhudi za kuimarisha elimu ya umma.

Biashara huzingatia suala la mtaji wa binadamu katika utetezi wao wa mageuzi katika elimu. Shirikisho la Biashara la Japani, sawa na watetezi thabiti wa uchumi ulimwenguni, limetoa mapendekezo ya sera ya elimu ambayo yanatetea usasa na ustadi unaoambatana na karne ya 21. Baadhi wamekosoa mapendekezo hayo wakisema yanatofautiana na mazoea ya kuajiri na mafunzo ya waajiri. Shirika la Global Business Coalition for Education limetoa wito kwa wanachama wake kuangazia sana elimu kisiasa kupitia utaalamu, uongozi na rasilimali zao. Wakosoaji wanapinga kuwa njia bora ya kusaidia elimu ya umma itakuwa kujihusisha kwa dhati na kampeni dhidi ya kukwepa na kukosa kulipa kodi. Wasiwasi pia umeelezwa kuhusu jinsi kampuni za teknolojia ya elimu, ambazo hutumia mbinu za uuzaji kuuza bidhaa za serikali kwa njia ambazo haziambatani na manufaa ya umma, zilizidisha juhudi zao wakati wa janga la COVID-19 na mabadiliko ya masomo kuendelea kutoka nyumbani.

UTUNZAJI NA ELIMU YA CHEKECHEA

Wahusika wasio wa serikali wanaongoza huduma za utunzaji na elimu kwa watoto wa chini ya miaka 3. Katika nchi 33 za kipato cha juu, taasisi za binafsi ziliwakilisha asilimia 57 ya jumla ya uandikishaji mnamo 2018. Katika Australia, Ayalandi, Uholanzi, Nyuzilandi na Uingereza, sekta binafsi inayolenga faida ndiyo inayohusika sana. Nchini Ujerumani katika mwaka wa 2017, asilimia 73 ya uandikishaji ilikuwa katika taasisi za binafsi lakini ni asilimia 3 tu ya watoa huduma waliokuwa wa faida. Katika nchi 33 za kipato cha kati, wahusika wasio wa serikali waliwakilisha asilimia 46 ya uandikishaji wa watoto wa chini ya miaka 3, viwango vikiwa karibu na sifuri katika Shirikisho la Urusi hadi asilimia 100 nchini Uturuki. Ni nchi chache tu, ikiwemo El Salvador, ambazo zimebadilisha na kuongeza utoaji wa elimu wa serikali. Nchi za Amerika ya Kusini, ikiwemo Kolombia, Gwatemala na Peru, zimekubali mipango midogo ya utunzaji wa watoto, iliyojikita katika jamii. Utoaji wa huduma unaosimamiwa na waajiri, ambao unapatikana sana katika nchi tajiri, unaibuka polepole katika nchi maskini. Changamoto kuu ni kwamba ajira katika sekta rasmi huchangia asilimia 30 tu ya ajira katika nchi za kipato cha chini na cha kati.

Watendaji wasio wa serikali ni maarufu zaidi katika elimu ya chekechea kuliko elimu ya msingi. Kati ya mwaka wa 2000 na 2019, idadi ya taasisi binafsi katika uandikishaji wa jumla wa elimu ya chekechea iliongezeka kutoka asilimia 28.5 hadi asilimia 37, na kufikia asilimia 55 huko Mashariki na Kusini Mashariki mwa Asia. Nchini Uchina, chini ya sera ya 'kutembea kwa miguu miwili', kiwango cha taasisi binafsi kiliongezeka kutoka asilimia 31 hadi 57. Nchini Viet Nam, kiwango cha uandikishaji katika taasisi binafsi kilishuka kutoka asilimia 60 mwaka wa 2003 hadi asilimia 12 mwaka wa 2014. Viwango huwa tofauti, kuanzia chini ya asilimia 1 katika nchi za Ulaya Mashariki, ikiwemo Ukraini, hadi zaidi ya asilimia 95 katika Karibi (k.m. Antigua na Barbuda) na Pasifiki, ambapo utoaji wa elimu huwa ama wa kijamii (k.m. Vanuatu) au unahusishwa na shughuli za kidini (k.m. Samoa). Afrika ya Kaskazini na Asia ya Magharibi, ikiongozwa na Algeria na Misri, ndilo eneo lililorekodi kiasi kikubwa cha kushuka kwa taasisi binafsi katika uandikishaji wa elimu ya chekechea, kutoka asilimia 53 mwaka wa 2000 hadi asilimia 36 mwaka wa 2019. Kwa upande mwingine, kati ya 2000 na 2018, kiwango cha taasisi binafsi kiliongezeka nchini Israeli kutoka asilimia 5 hadi asilimia 36 na nchini Kuwait kutoka asilimia 26 hadi asilimia 45.

Gharama ya utoaji wa elimu ya chekechea isiyo ya serikali inaweza kuwa kubwa mno kwa walio maskini zaidi. Tafiti za kaya zinaonyesha kuwa data ya usimamizi ilipunguza kiwango cha uandikishaji wa taasisi zisizo za serikali, katika nchi sita kati ya saba za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa asilimia 20, kwa wastani. Utoaji wa elimu usio wa serikali umeshughulikia sana mahitaji katika maeneo ya mijini, ambapo huduma kama hizo huwa zinapatikana kwa kawaida, na kutoka kwa kaya tajiri, ambazo zinaweza kuzimudu. Kama sehemu ya matumizi ya kila mwaka ya kaya, elimu ya chekechea ya binafsi inachukua asilimia 6 kwa walio matajiri zaidi na asilimia 17 kwa walio maskini zaidi nchini Ghana; nchini Ethiopia, takwimu hizo ni asilimia 4 na asilimia 21.

Utoaji wa huduma usio wa serikali ni changamoto kwa usimamizi na udhibiti. Wingi wa wahusika wasio wa serikali hufanya usimamizi kuwa mgumu. Nchi ya Kambodia ina kanuni na amri tofauti kwa ajili ya shule za chekechea za jamii. Nchini Sri Lanka, kutokuwepo kwa mfumo wa udhibiti wa sekta mbalimbali kunamaanisha kuwa wigo wa kazi wa wizara kadhaa (elimu, afya, na masuala ya wanawake na watoto) na mabaraza ya majimbo unapishana. Huko Lagos, Nigeria, uwezekano wa wizara ya elimu ya serikali kukagua shule ya chekechea ya binafsi ulikuwa juu ikiwa shule hiyo ilitoza ada ya juu (asilimia 68) kuliko ikiwa ilitoza ada ya chini (asilimia 48). Huko Nairobi, Kenya, shule za jamii hukaguliwa mara nyingi kuliko shule za kidini, za uhisani au za faida.

Ubora wa watoa huduma wasio wa serikali unatofautiana sana. Katika nchi nyingi za kipato cha chini na cha kati, waelimishaji binafsi huwa hawajaandaliwa vya kutosha na wana fursa chache za kujiendeleza kitaaluma wakilinganishwa na wenzao wa sekta ya umma. Ni asilimia 8 tu ya walimu binafsi na asilimia 75 ya walimu wa umma wa shule za chekechea ambao hufanya mpango wa mafunzo wa Huduma ya Elimu ya Ghana, kwani hakuna masharti ya chini kwa walimu binafsi. Matumizi ya Kiingereza kama lugha ya kufundishia katika shule za chekechea zisizo za serikali, kama ilivyo nchini Brazil, ni mfano wa mvutano kati ya mitaala inayofaa katika ukuaji na mitazamo maarufu ya ubora.

Ni nchi chache za kipato cha chini na cha kati ambazo zina taratibu za kuhakikisha ubora ambazo zinazingatia zaidi ya mahitaji ya usimamizi. Nchini Jamaica, ambapo utoaji wa huduma za elimu sanasana umo mikononi mwa wahusika wasio wa serikali, wizara ya elimu inahitaji wakaguzi waliohitimu; wafanyakazi wengine hufanya ziara za ufuatiliaji za kila mwezi kulingana na viwango 12 vya kitaifa, vinavyojumuisha ushirikiano na uhusiano kati ya watoto, walimu, wazazi, walezi na wanajamii. Nchi ya Ufilipino inafuatilia viwango na ustadi wa kitaifa kupitia Orodha ya Ukaguzi wa Maendeleo ya Watoto ya Ufilipino iliyothibitishwa na serikali.

Wahusika wasio wa serikali hubuni na kutetea ECCE (Utunzaji na Elimu ya Chekechea). Kihistoria, wanaelimu waliojitolea walifanya kazi nje au pembezoni mwa mfumo rasmi wa elimu ya umma kutekeleza maono yao ya mafunzo yaliyolenga watoto. Watafiti wa kitaaluma wameangazia ufanisi wa muda mrefu wa programu za elimu ya watoto, wakihimiza mamlaka ya umma kupanua programu hizo. Wahusika wasio wa serikali hutetea watoto waliotengwa, wakishirikiana na akina mama katika magereza nchini Chile, wazazi maskini wanaofanya kazi nchini Ufilipino na watoto katika taasisi nchini Romania. Mashirika kama vile Bernard van Leer Foundation, Aga Khan Foundation na Open Society Foundations yamehamasisha utetezi na usaidizi wa ECCE.

ELIMU YA JUU

Karibu nchi zote zinahakikisha utoaji wa elimu ya juu kupitia mseto wa wahusika wa serikali na wale wasio wa serikali. Karibu asilimia 33 ya wanafunzi wa elimu ya juu wamejiunga na taasisi binafsi duniani kote, huku sehemu ya juu ikiwa katika Asia ya Kati na Kusini na Amerika ya Kusini na Karibi. Ukuaji katika utoaji huduma usio wa serikali unashughulikia mahitaji mbalimbali. Taasisi za kidini au kitamaduni zinahusishwa na historia na utamaduni, zikitimiza mahitaji ya elimu 'tofauti'. Taasisi za matabaka ya juu hujitokeza ili kukabiliana na mahitaji ya elimu 'bora', mara nyingi kutoka kwa matajiri. Hatimaye, taasisi ndogo, zisizo za kidini zimeongezeka hivi karibuni katika kukabiliana na mahitaji ya elimu 'zaidi' ya juu, hasa katika muktadha wa bajeti finyu za umma.

Taasisi zisizo za serikali zinaathiri ubora wa mfumo. Taasisi ndogo zinazotoza ada huwa zinatoa mafunzo katika nyanja chache, hasa yanayoegemea upande wa ufundi. Nchini India, karibu asilimia 40 ya vyuo binafsi hutoa mafunzo ya uwanja mmoja tu, kwa ujumla elimu. Wahadhiri wa taasisi zisizo za serikali wana uwezekano mdogo wa kuwa na nafasi za kazi za kudumu – chini ya asilimia 20 nchini Senegal - na mara nyingi huwa ni maprofesa wanaofanya kazi katika taasisi za umma. Nchini Malaysia, idadi ya wahadhiri wenye kazi katika taasisi zingine inaweza kufika asilimia 80 ya wafanyakazi katika taasisi ndogo na mpya zisizo za serikali. Lengo la faida huongeza changamoto za ziada za ubora zinazohusiana na ukubwa wa mgao katika soko na kupatia faida kipaumbele badala ya kuboresha masomo.

Utoaji wa elimu usio wa serikali unaibua wasiwasi kuhusu usawa. Katika nchi za kipato cha juu na cha kati, sehemu kubwa ya wahusika wasio wa serikali katika uandikishaji wa jumla huhusishwa na ukosefu mkubwa wa usawa katika mahudhurio. Nchini Urugwai, zaidi ya asilimia 75 ya mwanafunzi katika taasisi zisizo za serikali hutoka katika familia tajiri, ikilinganishwa na chini ya asilimia 40 katika taasisi za umma. Bado, taasisi zisizo za serikali zinaweza kusaidia vikundi vilivyo katika hatari ya kutengwa, vipate elimu. Huko Saudi Arabia, wamepanua ufikiaji kwa wanawake kwa kutoa kozi za wanawake pekee, huku nchini Malaysia wanatoa nafasi za kufikia kwa Wachina asili na Wahindi waliozuiwa kuingia taasisi za umma kutokana na madaraja ya kikabila. Hata hivyo, utoaji huo wa kando unaweza kuwa hatari kwa mshikamano wa kijamii.

Mifumo ya udhibiti huwa inaakisi maoni ya serikali kuhusiana na wahusika wasio wa serikali. Kanuni kali zinahusishwa na kutoaminiana, huku mtazamo mzuri zaidi wa wahusika wasio wa serikali unaweza kusaidia uidhinishaji, ufuatiliaji na hata ufadhili wa umma. Katika baadhi ya nchi, taasisi za faida huwekewa mwongozo mkali zaidi – zinaweza kupigwa marufuku kabisa, kama ilivyo nchini Argentina na Chile, au kuwekewa vizuizi kwenye ugawaji wa bajeti, kama vile kikwazo cha faida cha asilimia 10 nchini Ufilipino. Kwa ujumla, mifumo ya uhakikisho wa ubora imesaidia nchi kufunga taasisi zinazojihusisha na mazoea ya kibiashara ya udanganyifu au kutoa huduma za ubora wa chini. Mwaka wa 2017, Tume ya Elimu ya Juu ya Pakistan ilitambua taasisi 153 haramu zilizokuwa zinaendesha shughuli zake nchini humo. Lakini rasilimali

za kuidhinisha na kufuatilia taasisi zisizo za serikali mara nyingi hazipo.

Kanuni zinazoendeleza usawa hazipatikani sana ikilinganishwa na sheria za usimamizi. Mgao au vigezo maalum vya uandikishaji vilivyoundwa ili kuboresha nafasi za vikundi visivyojiweza kufikia elimu ya juu huwa havijumuishi watoa huduma wasio wa serikali kila wakati. Vinapowajumuisha, kama nchini India, kwa kawaida huwa vinajumuisha tu taasisi zinazopokea ufadhili wa umma. Vighairi ni pamoja na kulazimisha taasisi zisizo za kiserikali kutoa misaada au ufadhili wa kimasomo kwa baadhi ya wanafunzi, kama ilivyo Bolivia na Ekwado, na kudhibiti ada ya wanafunzi, kama ilivyo Azerbaijan na Kenya.

Njia za ufadhili wa taasisi zisizo za serikali zina athari kubwa za ubora na usawa. Taasisi nyingi zisizo za serikali, hasa zile ambazo ni ndogo na zisizo za takaba la juu, hutegemea sana ada ili kujifadhili. Lakini pia serikali husaidia kugharamia taasisi zisizo za kiserikali katika nchi nyingi. Baadhi ya wahadhiri wanapewa ruzuku kama watumishi wa umma nchini Indonesia, na mfuko maalum umewekwa kwa ajili ya taasisi zisizo za serikali nchini Thailand. Uwezo wa kupata fedha za umma unaweza kuboresha utoaji wa elimu wa taasisi zisizo za serikali kwa kuhimiza miradi ya utafiti au, ikiwa kuna masharti, kushinikiza taasisi kufikia viwango vya ubora au usawa.

Familia zimechukua sehemu kubwa ya ufadhili wa elimu ya juu, na kuongeza hitaji la msaada wa serikali na usio wa serikali. Serikali zinaweza kutoa ruzuku ya ada kwa taasisi zisizo za serikali, kama ilivyo Brazil na Chile, au kutoa ruzuku kwa programu za mikopo ya wanafunzi, zinazopatikana katika nchi zaidi ya 70 kwa wanafunzi wote wa elimu ya juu. Wahusika wasio wa serikali husaidia kaya kufidia gharama kupitia ufadhili wa masomo unaolipwa na makampuni, mashirika mengine, mashirika yasiyo ya kiserikali na wahisani, na pia kwa kutoa mikopo ya wanafunzi au makubaliano ya kugawana mapato.

Wahusika wasio wa serikali hufadhili taasisi kwa njia zingine kando na ada. Njia za kawaida ni pamoja na kushiriki katika shughuli za soko kama vile ukodishaji wa ardhi, kuuza bidhaa na huduma, na kutoa mtaji kupitia mikopo na dhamana. Kufikia katikati mwa 2020, utoaji wa dhamana wa vyuo vikuu ulimwenguni kote ulikuwa umefikia dola za Marekani bilioni 11.4, zaidi ya maradufu ya kiasi cha 2019. Wafadhili na wahisani pia wanawakilisha chanzo muhimu cha mapato kando na ada, wakichangia zaidi ya nusu ya jumla iliyokusanywa na taasisi za elimu ya juu nchini Marekani mnamo 2020.

Wahusika wasio wa serikali huathiri elimu ya juu kupitia njia mbalimbali. Baadhi ya njia, kama vile ushirikiano katika utafiti, ushawishi, mageuzi ya usimamizi sawa na ya kibiashara na utetezi, zinaweza kusaidia kuongeza uwazi na kuimarisha sekta hiyo. Njia zingine, kama vile michango mikubwa kutoka kwa taasisi za faida kwa wanasiasa (k.m. Brazil na Marekani), zinaweza kusababisha ushawishi usiofaa katika utungaji wa sera na kudhoofisha uhuru wa taasisi.

ELIMU YA KIUFUNDI NA YA WATU WAZIMA

Wahusika wasio wa serikali wamesaidia kupanua utoaji wa elimu ya kiufundi. Kote ulimwenguni, asilimia 38.5 ya wanafunzi katika elimu ya baada ya sekondari na isiyo ya juu, walichagua taasisi za binafsi mnamo 2019. Katika nchi za OECD, asilimia 44 ya wanafunzi katika mipango ya kiufundi ya kipindi kifupi waliandikishwa katika taasisi za binafsi. Ushirikiano na wahusika wasio wa serikali una lengo la kufanya mifumo ya elimu na mafunzo ya kiufundi (TVET) ishughulikie zaidi mahitaji ya soko la ajira na kuongeza rasilimali na uwezo wao, hata katika nchi zenye mifumo ya TVET ya umma iliyounganishwa. Katika miktadha mingine, wahusika wasio wa serikali wameongeza utoaji wa elimu ya kiufundi kupitia njia za jadi, mipango huru ya mafunzo na ubia wa wadau wa umma na wa binafsi, ambao sanasana unaratibiwa na serikali. Katika nchi maskini, wahusika wasio wa serikali hutoa ufikiaji wa TVET wenye usawa kwa vikundi visivyojiweza

Waajiri hushiriki katika uanagenzi rasmi na usio rasmi. Utafiti wa Mpito kutoka Shule hadi Kazi wa Shirika la Kazi Duniani uligundua kuwa chini ya mshiriki 1 kati ya washiriki 5 wa kati ya miaka 15 hadi 35 katika nchi 33 walishiriki katika angalau kipindi kimoja cha kupata mafunzo katika muktadha wa kazi kama sehemu ya elimu yao. Kiwango cha chini cha kushiriki katika nchi za kipato cha chini kinaweza kuhusishwa na ukosefu wa urasmi wa soko la ajira na mifumo ya mafunzo. Bila kudhibitiwa na kutambuliwa vya kutosha, vichochezi vinavyohusiana na uanagenzi vinaweza kufutika . Mashirika ya upatanishi yanaweza kuandaa mazungumzo na waajiri, kuboresha ufunzaji na kuhakikisha ulinganisho unaofaa, hasa katika nchi ambazo hazina taratibu thabiti ya uanagenzi.

Nafasi za kuendelea kuimarisha ujuzi hutolewa sanasana na waajiri binafsi. Wakati masomo rasmi ya TVET yanalenga kazi zilizo katika hatari ya kufanywa na mashine, kufunza ujuzi mpya na kuongeza ujuzi hufanyika nje ya elimu ya jadi. Mafunzo yasiyo rasmi na yanayofadhiliwa na mwajiri yanapatikana; kile kinachotolewa kinahusiana moja kwa moja na ukubwa wa kampuni. Matokeo kutoka Programu ya Upimaji Ujuzi ya STEP ya Benki ya Dunia yanaonyesha kuwa waajiri wanapendelea mafunzo yanayotolewa kazini badala ya programu za nje zinazotolewa na watoa huduma rasmi wa umma au wa binafsi.

Usimamizi shirikishi katika mifumo ya kukuza ujuzi ni changamoto. Mifumo ya TVET imebaki chini ya serikali kuu. Mifumo ya kitaifa ya kufuzu katika nchi zaidi ya 150 inalenga kufanya usimamizi wa TVET kuwa shirikishi zaidi na unaotimiza lengo lililonuiwa, ingawa kuboresha uwazi na ufaafu wa ujuzi bado ni kipaumbele kwa mamlaka ya umma. Ufanisi wa mifumo ya TVET unakwamishwa na njia za kuhakikisha ubora ambazo hazijatekelezwa kikamilifu. Maingiliano kati ya sekta binafsi na ile ya elimu huwa yanazingatia utambuzi wa ujuzi badala ya kubuni mtaala. Mifumo ya ujuzi ambayo inakabiliana vizuri na mabadiliko ya kiuchumi ni ile inayotegemea njia za utatu, na kushirikisha wahusika wa kijamii na kiuchumi. Ushirikiano wa umma na sekta binafsi unaozingatia maarifa kupitia mabaraza ya ujuzi umeanzishwa ili kuboresha uelewa wa mahitaji ya soko la ajira.


Mifumo ya ukuzaji ujuzi hutegemea ufadhili wa serikali na usio wa serikali. Mbali na mgao wa moja kwa moja wa serikali, mifumo ya TVET inataka kupanua njia za kupata ufadhili kupitia ushuru wa mafunzo maalum au fedha zinazohusisha makampuni. Wahusika wasio wa serikali pia wamehusika moja kwa moja kupitia ununuzi wenye ushindani, lakini matokeo yamekuwa mseto. Waajiri wanahimizwa kutoa mafunzo kupitia programu za ruzuku. Bado, makampuni hayawekezi vya kutosha katika mafunzo, kwani motisha wa kufanya hivyo uko chini ukilinganishwa na motisha ya kutafuta ujuzi unaohitajika moja kwa moja kutoka kwenye soko la ajira. Serikali hutoa vichochezi kwa watu binafsi kwa kulipia gharama za mafunzo za moja kwa moja au zisizo za moja kwa moja kupitia haki au akaunti za mafunzo za mtu binafsi.

Mashirika yasiyo ya kiserikali na yale ya jamii ndiyo mengi katika mipango ya mafunzo ya watu wazima. Kupitia vituo vya kujifunza vya jamii, programu za mafunzo ya kusoma na kuandika na nyingine kama hizo, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya kiraia hufikia vikundi vya watu wazima walio katika mazingira magumu, ambavyo kwa kawaida vilikuwa vimetengwa na mifumo ya elimu rasmi. Wakati mwingine, serikali hutegemea huduma zao kutoa programu za kitaifa za masomo ya watu wazima na mipango ya kuwapa watu fursa ya pili. Katika miktadha mingine, vikundi kama hivyo vimepinga juhudi za serikali za kutoa elimu ya watu wazima, hasa Amerika Kusini, k.m. kufunza lugha zisizo kuu katika masomo ya watu wazima. Katika miktadha mingine, vikundi hivyo huathiriwa na vipaumbele vya wafadhili. Kushiriki kwao katika juhudi za serikali za kubuni sera bado ni finyu, ingawa katika Afrika ya magharibi na kati , ugatuzi wa 'faire-faire' na mkakati wa utoaji wa kandarasi umeleta matokeo mazuri, huku serikali ikisimamia na kugawa rasilimali wakati wahusika wasio wa serikali wanasimamia utoaji wa elimu.

Sekta binafsi imepanua jukumu lake katika elimu ya watu wazima, hasa katika ufunzaji wa lugha. Makampuni binafsi yanaweza kujihusisha na elimu ya watu wazima kupitia maendeleo ya jamii, mara nyingi kama sehemu ya mipango ya uwajibikaji wa kijamii au utoaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano.

Umuhimu unaoendelea kuongezeka wa kujifunza na kutathmini lugha umevutia makampuni ya faida. Karibu asilimia 40 ya wanafunzi wa Kiingereza nchini Argentina na Peru wanasomea taasisi za lugha za binafsi. Kujifunza lugha kupitia simu pia kunaenea, lakini ufanisi wake unazua mjadala.

MAPENDEKEZO



Mbali na uainishaji rahisi wa umma na binafsi, kuna aina mbalimbali za shule zisizo za serikali. Isitoshe, jukumu la wahusika wasio wa serikali ni zaidi ya utoaji wa masomo na linajumuisha hatua zingine nyingi katika viwango mbalimbali vya elimu na kupitia njia nyingi za ushawishi. Swali kwa watunga sera halihusu tu ikiwa ushiriki wa wahusika wasio wa serikali katika elimu unakidhi viwango vya ubora vilivyokubaliwa, lakini pia jinsi wahusika hao wanavyosaidia au kuzuia juhudi za kuhakikisha usawa na ujumuishaji katika elimu.

Mielekeo miwili ya kimkakati, inayohusiana na ufadhili na utoaji wa elimu, inajitokeza kuhusiana na kazi ya serikali ya kulinda na kutimiza haki ya elimu. Kwanza, serikali iliahidi mnamo 2015 kwamba watoto na vijana wote watakuwa na fursa ya kupata elimu ya bure; elimu ya mwaka mmoja ya chekechea na miaka 12 ya elimu ya msingi na sekondari iliyofadhiliwa na serikali. Hata hivyo, moja kati ya nchi tatu zinatenga chini ya asilimia 4 ya Pato la Taifa na asilimia 15 ya jumla ya matumizi ya serikali kwa elimu, hivyo nchi nyingi hazilinganishi ahadi hii na kiasi cha pesa

kinachohitajika. Pili, serikali zinahitaji kuamua jukumu lao katika kutoa na kusimamia elimu litakuwa kubwa kiasi gani. Mitazamo yao ukilinganishwa na uchaguzi wa shule na wahusika wasio wa serikali hutofautiana sana.

Wahusika mbalimbali wasio wa serikali wamejitokeza zaidi katika hali nyingi za elimu. Biashara huchagua ikiwa elimu ni shughuli yenye faida na jinsi ya kuuza bidhaa na huduma zao, lakini pia yule wanayewajibikia: wanahisa tu au wengine pia? Mashirika yasiyo ya kiserikali na yale ya kiraia huchagua vipaumbele na kuamua jinsi ya kuvishughulikia: Je, mashirika haya yanafaa kujaza mapengo au yanafaa kutetea serikali kufanya hivyo? Mashirika pia huweka vipaumbele na kuchagua jinsi ya kushawishi jamii na jinsi ya kufanya kazi kwa ukaribu na mifumo ya elimu. Walimu na mashirika yao hufanya uchaguzi ambao unaweza kuimarisha au kuharibu imani katika mifumo ya elimu ya umma.

Kauli mbiu ya ripoti – Ni nani anayechagua? Ni nani anayepoteza? – ni mwaliko kwa watunga sera kudadisi uhusiano na wahusika wasio wa serikali katika suala la machaguo ya msingi: kati ya usawa na uhuru wa kuchagua; kati ya kuhimiza uchukuaji hatua (yaani kuimarisha ubora kote katika mfumo) na kuweka viwango (yaani kuimarisha ubora kwa wanafunzi wote); kati ya vikundi vya uwezo na mahitaji tofauti; kati ya ahadi zao za sasa (yaani miaka 12 ya elimu ya bure chini ya lengo la 4 la Maendeleo Endelevu) na zile ambazo zitatimizwa hatua kwa hatua (k.m. elimu ya baada ya sekondari); na kati ya elimu na sekta zingine za kijamii.

Kwa kuzingatia mawazo haya, mapendekezo yafuatayo yalibuniwa ili kusaidia wito wa #RightttheRules kuhakikisha kuwa usawa katika elimu unalindwa katika ufadhili, ubora, usimamizi, uvumbuzi na utungaji wa sera. Lengo kuu ni kutumia michango ambayo wahusika wasio wa serikali wanaweza kufanya ili kutoa elimu bora bila kutelekeza usawa. Kujaribu kufikia uwezo huu pia kunaweza kuchochea serikali kushughulikia kwa makusudi viwango vya chini vya ubora na ukosefu wa usawa katika utoaji wa elimu kwa umma. Mapendekezo yanalenga hasa serikali, ambazo zinahitaji kutoa majibu bayana kwa maswali matano ya msingi kwa kuzingatia mtazamo wa usawa na ujumuishaji. Walakini, pia yanakusudiwa kutumiwa kama zana ya utetezi na wahusika wote wa elimu waliojitolea kusaidia katika juhudi za kufikia lengo la 4 la Maendeleo Endelevu. Kwa hivyo, mapendekezo haya yanataka wahusika wote, wa serikali na wasio wa serikali, kuzingatia wito wa #RightbytheRules.

1. JE, KUGHARAMIA ELIMU KUNAPENDELEA BAADHI YA WANAFUNZI NA KUWATENGA WENGINE?

Timiza ahadi ya kufanya mwaka 1 wa elimu ya chekechea na miaka 12 ya elimu ya msingi na sekondari kupatikana bure – lakini si lazima kufadhiliwa na serikali kumaanishe kutolewa na serikali ikiwa usawa unaweza kuhakikishwa.



Serikali zinapaswa kufanya elimu bora iwe ya bure popote inapopatikana. Zinahitaji kuhakikisha kuwa kaya hazilipii bidhaa na huduma za elimu ambazo nchi zao zimeahidi kutoa bila malipo.

Serikali zinahitaji kufuatilia matumizi ya elimu yanayogharamiwa na familia, kupitia tafiti za mapato na matumizi ya kaya. Mara nyingi serikali hupuuza gharama ambazo hazijarekodiwa vizuri, ambazo huongeza ukosefu wa usawa.

Watoa huduma wote, wa serikali na wasio wa serikali, lazima watoe hali sawa kwa wanafunzi. Ahadi kwamba elimu itafadhiliwa na serikali haimaanishi kuwa elimu yote lazima itolewe na serikali. Lakini taasisi zote za elimu zinapaswa kuchukuliwa kama sehemu ya mfumo mmoja wenye sheria sawa, msaada sawa wa kifedha na njia sawa za usimamizi.

Majaribio yoyote ya kupanua utoaji wa huduma za elimu yanapaswa kubuniwa kwa njia ambayo inahakikisha usawa. Kutoa kandarasi za usimamizi wa shule za umma, kutoa ruzuku za gharama za uendeshaji wa shule za binafsi au kutoa ufadhili kwa kaya ili waweze kuhudhuria shule waliyojichagulia kunaweza kuwanufaisha wanafunzi ambao wametoka katika familia zinazojiweza.


Shule hazipaswi kuchagua wanafunzi. Nchi zimeahidi kutobagua katika elimu, kanuni ambayo lazima ionekane katika sera za kuingia shuleni. Aidha, haki ya familia na wanafunzi kuchagua shule haipaswi kuongeza ukosefu wa usawa.

Watoa huduma wasio wa serikali wanaofadhiliwa na serikali hawapaswi kutoza ada yoyote. Ingawa nchi zote zinapaswa kulenga kuhakikisha kuwa elimu ya chekechea, ya msingi na ya sekondari ni ya bure, nchi nyingi hazijaweza kufikia hatua hii. Hata taasisi binafsi zinazotegemea serikali huwa zinatoza ada.

Upataji faida hauendani na ahadi ya kuhakikisha elimu ya chekechea, ya msingi na ya sekondari inatolewa bure. Kudhibiti au kupiga marufuku upataji wa faida kunaweza kutumika kushughulikia sera za uchaguzi wa shule ambazo zinazidisha ukosefu wa usawa.

2. 2. JE, WANAFUNZI WOTE WANAPOKEA UBORA WA ELIMU WANAOSTAHILI, AU BAADHI YAO WANADANGANYWA?

Weka viwango vya ubora vinavyotumika kwa taasisi zote za elimu, za serikali na zisizo za serikali



Serikali zinahitaji kuweka viwango vya ubora vinavyotumika kwa taasisi zote za elimu. Viwango vya ubora, vinavyozingatia bidhaa na huduma zinazotolewa na pia matokeo, hulinda wale ambao wanaweza kuathirika zaidi. Vinapaswa pia kushughulikia usalama na ujumuishaji. Vinapaswa kuzingatia mahali shule zilipo na kuzisaidia kuwa bora. Mafanikio yake yanapaswa kutathminiwa kwa kila shule, ya serikali na isiyo ya serikali, na kuripotiwa hadharani.

Walimu wanapaswa kuthaminiwa kama wataalamu katika shule zote. Sifa za walimu na fursa za kujiendeleza kitaaluma hazipaswi kutofautiana kulingana na mtoa huduma. Masoko ya ajira ya walimu yaliyogawanyika na tofauti kubwa katika hali na malipo ya walimu ni ishara thabiti za mfumo wa elimu usiofanya kazi ipasavyo. Serikali zinahitaji kuendelea kushughulikia sababu zote zinazoleta ukosefu kama huo wa usawa.


Njia za kuhakikisha ubora zinahitaji kuwa zimewekwa ili kufuatilia na kutekeleza viwango. Usimamizi wa serikali kupitia ukaguzi wa shule, tathmini na ukadiriaji wa mafunzo zinapaswa kuwa za kawaida, bila kujali mtoaji huduma. Njia hizi zinapaswa kuzingatia uwezo wa serikali wa kutekeleza.

Nchi zinahitaji michakato thabiti zaidi ya kuhakikisha ubora katika elimu ya ufundi na ya juu. Serikali zinapotoa ruzuku kwa watu binafsi au mikataba kwa makampuni ili kuendeleza mafunzo, zinahitaji kulinda wale wasiojiweza, ambao wako katika hatari ya kuhadaiwa. Vyuo vikuu vya faida vimefanyiwa uchunguzi kwa kutoa elimu ya ubora wa chini zaidi na kujihusisha katika shughuli zisizokubalika.

Serikali zinahitaji kuzuia masomo ya ziada ya kibinafsi kuathiri ubora na usawa wa mfumo. Majibu ya sera hutofautiana kuanzia masharti ya kibali cha kufundisha hadi kuwa na rejesta za mtandaoni ili kuhakikisha usimamizi bora. Chaguo lingine pia ni kupiga marufuku ila hili linaweza kusababisha masoko yasiyo rasmi. Kipaumbele kinapaswa kuwa kushughulikia sababu za msingi, kama vile malipo duni ya walimu na mitihani ya mwisho yenye matarajio ya juu.

3.JE, KANUNI ZINAFAA NA ZINAWEZEKANA, AU ZINA MATOKEO YASIYOTARAJIWA AMBAYO HUWAUMIZA WANAFUNZI WASIO NA UWEZO?

Anzisha michakato ya kawaida ya ufuatiliaji na usaidizi, ambayo inatumika kwa taasisi zote za elimu, za serikali na zisizo za serikali



Serikali zinahitaji maono na mfumo bayana wa jinsi zinavyotaka kuwashirikisha wahusika wasio wa serikali na kuwasilisha maono haya kupitia kanuni. Kanuni hazipaswi kuzingatia maelezo ya kiusimamizi na viwango vya hatua zinazofaa kuchukuliwa ambavyo haviambatani na uhalisia, bali zinafaa kuzingatia michakato ya elimu na matokeo, na zinafaa zikaguliwe na zirekebishwe mara kwa mara kwa njia ya uwazi na shirikishi, huku shule za serikali na zisizo za serikali zikialikwa kuchangia.

Watoa huduma za elimu wanapaswa daima kudhibitiwa kama taasisi za elimu na mamlaka ya elimu, na kamwe hawafai kudhibitiwa kama taasisi za kibiashara na wasimamizi wa soko. Watoa huduma wengine katika utunzaji na elimu ya chekechea, masomo ya ziada ya kibinafsi na mafunzo ya ufundi wanadhibitiwa kama biashara. Vile vile, watoa huduma wengine wanasimamiwa na wizara ya ulinzi wa jamii au na mamlaka za kidini.

Kanuni zinahitaji kuwa rahisi, zenye uwazi na ufanisi. Kitendawili ni kwamba uwezo wa kudhibiti uko chini kabisa katika miktadha ambapo unahitajika zaidi, na ambapo uwezekano wa ufisadi uko juu. Pale ambapo uwezo wa kufuatilia na kutekeleza sheria ambazo ni ngumu kutimiza unapokosekana, kanuni zinakuwa hazina maana na hazina manufaa.

Serikali zinahitaji kuangalia visababishi vya jambo wanalotaka kudhibiti kwa ukweli. Michakato ya ufuatiliaji na usaidizi inapaswa kuwa ya kawaida, hivyo kuonyesha kuwa serikali zinajali elimu ya watoto wote, bila kujali aina ya shule wanayohudhuria. Serikali pia zinahitaji kujenga uhusiano wenye uaminifu na watoa huduma wasio wa serikali, huku wakiwasilisha vichochezi vinavyofaa kwao ili waendeshe shule zao kwa ufanisi.

4. JE, MAWAZO MAZURI KUHUSU ELIMU YANAENDELEZWA AU YANAKOMESHWA?

Kuwezesha kuenea kwa uvumbuzi kupitia mfumo wa elimu kwa manufaa ya wote



Watunga sera wanapaswa kuwa na uwezo wa kutambua uvumbuzi na kupatia mawazo mazuri wakati na nafasi ya kuendelezwa. Hakuna mwenye ukiritimba wa mawazo mazuri. Elimu ni juhudi ya kijamii na ni mfumo changamano. Changamoto kwa watunga sera ni kuhimiza uvumbuzi, hasa wakati umma kwa ujumla unaweza kupendelea utiifu kuliko majaribio.

Serikali inapaswa kufanya kazi kwa ushirikiano na wahusika wote ili kujenga mfumo wa elimu ambao unawafaa wote, huku mashauriano yakipewa kipaumbele. Desturi za uaminifu zinahitaji kujengwa ili kuendeleza uvumbuzi. Kuhakikisha hali na kutoa majukwaa kwa wahusika wengi kushauriana na kushirikiana kunaweza kusaidia mfumo wa elimu ya umma kufaidika na maoni tofauti na vyanzo tofauti vya utaalamu ili kuendelea kuwa muhimu.

Mwanzo, serikali zinahitaji kuendeleza uvumbuzi katika mfumo wa elimu ya umma. Zinahitaji kuonyesha kwamba zimejitolea kuhakikisha ubora. Zinapaswa kufuatilia masomo na kanuni zake, kutathmini ni wapi mazoea mazuri yanafanyika, kutoa rasilimali zinazowezesha watendaji kubadilishana uzoefu, kufanya majaribio ya mawazo mazuri na kuyapanua.

Serikali pia inapaswa kutafuta mambo wanayoweza kujifunza kutoka kwa wahusika wasio wa serikali. Njia huru, zinazozingatia muktadha na rahisi za kufundisha wanafunzi waliotengwa zinaweza kutoa maarifa mapya, ambayo yanapaswa kufaidi serikali, huku zikitambua kuwa uwezo finyu unazizuia kufuatilia na kutathmini inavyofaa shule za serikali, sembuse zile zisizo za serikali.

Jukumu la serikali ni kuhakikisha mazingira yanayofaa ya kuwezesha ubunifu. Elimu haifai kuonekana kama soko ambapo 'wazalishaji' wa elimu wanashinda watoa huduma wengine. Badala yake, mawazo mapya yanahitaji kushirikiwa, kufanyiwa majaribio na, ikiwa yatathibitishwa, kupitishwa, huku serikali ikiyaeneza kupitia mfumo wa elimu na wahusika wasio wa serikali wakijitolea kuyaendeleza kwa manufaa ya wote badala ya kuchochewa na sababu za kiuchumi.

5. JE, SAUTI ZOTE ZINAPEWA FURSA SAWA ZA KUCHANGIA MJADALA WA UMMA KATIKA ELIMU?

Dumisha uwazi na uadilifu wa mchakato wa sera ya elimu ya umma ili kuzuia maslahi binafsi



Watunga sera wanahitaji kuzingatia maarifa na mitazamo kutoka kwa wadau wote. Lakini kama ambavyo watunga sera wanapaswa kuwa tayari kusikiliza maoni mbalimbali, ni muhimu pia kwa mawasiliano na viongozi wa umma kuhusu sheria, sera na kanuni za elimu, kuwa wazi. Baadhi ya wahusika wanaweza kuwa wanajitahidi kuongeza mgao wao wa soko au nguvu ya kisiasa badala ya manufaa ya umma.

Serikali zinahitaji kufuatilia na kulinda dhidi ya ushawishi unaolenga maslahi binafsi ili kuuzuia usiathiri sera ya umma kwa njia isiyostahili. Ili kudumisha imani katika michakato ya sera za umma, hatua mbalimbali za kukuza uwazi zinaweza kutumika, kulingana na uwezo, ikiwa ni pamoja na sheria za uhuru wa habari zinazohimiza ufumbuzi wa michango inayotolewa kwa vyama vya kisiasa na mikutano na viongozi waandamizi wa serikali. Pia sheria dhidi ya viongozi wa serikali ambao wanaondoka madarakani kuchukua nafasi ambazo zinaweza kuwapatia faida ya kibinafsi na kuzuia washawishi na wadhamini wao kuchukua ofisi za umma. Mapendekezo haya pia yanatumika kwa mashirika ya kimataifa ambayo yanahitaji sera wazi ya kushirikiana na wahusika wasio wa serikali. Sera hiyo inafaa ipatie kipaumbele usawa na ujumuishaji.

Ufuatiliaji wa elimu katika Malengo ya Maendeleo Endelevu

Tunapokaribia katikati ya kipindi cha kufikia Agenda ya 2030 ya Maendeleo Endelevu, kumekuwa na maendeleo muhimu katika kubuni mfumo wa ufuatiliaji na malengo ambayo nchi zimejiwekea. Hata hivyo, janga la COVID-19 limeleta vikwazo vikubwa kwa hali zote. Sio tu kwamba zana za kawaida zinazotumika kufuatilia maendeleo katika elimu zimeathirika, lakini malengo yenyewe huenda yakahitaji kufikiriwa upya.

NCHI ZIMEWASILISHA VIGEZO VYA KITAIFA VYA LENGO LA 4 LA MAENDELEO ENDELEVU


Mfumo wa Elimu wa Kuchukua Hatua wa 2030 ulizitaka nchi kutambua 'vigezo teule vinavyofaa vya vipindi vya kati (k.m. vigezo vya 2020 na vya 2025)' vya viashiria vya lengo la 4 la Maendeleo Endelevu ili kujua mchango ambao kila nchi itakuwa tayari kuchangia kwa ajenda ya kimataifa, kulingana na hali zao za mwanzo. Taasisi ya Takwimu ya UNESCO (UIS) na timu za Ripoti ya GEM zimefanya kazi kuhamasisha jumuiya ya kimataifa katika mwelekeo huo. Kufuatia uteuzi wa viashiria saba vya Lengo la 4 la Maendeleo Endelevu vya kutumiwa kama vigezo teule mnamo 2019, na mapendekezo ya Azimio la Mkutano wa Elimu wa Kimataifa mnamo Oktoba 2020 ili 'kuongeza kasi ya maendeleo na kupendekeza vigezo teule vinavyofaa vya viashiria muhimu vya SDG 4', nchi zilialikwa kuwasilisha takwimu za kitaifa za vigezo teule ifikapo Oktoba 2021 kwa vipindi vya 2025 na 2030. Asilimia 39 ya nchi ziliwasilisha takwimu. Asilimia nyingine 10 iliahidi kuwasilisha, huku ziada ya asilimia 14 ya nchi zikiwa ni wanachama wa Umoja wa Ulaya na Jumuiya ya Karibi ambao wana vigezo teule vya kikanda **(Mchoro wa 3).**

Taarifa juu ya viwango vya msingi na viwango vya vigezo teule vilivyowasilishwa vya 2025 na 2030 sasa imejumuishwa katika tovuti ya Global Education Observatory, sehemu mpya ya data inayohusiana na elimu. Ripoti ya GEM na taasisi ya UIS zitatoa ripoti ya msingi inayochambua matokeo ya mchakato huu mapema 2022. Ripoti hiyo itaangazia mahali ambapo nchi, kanda na ulimwengu unalenga kuwa. Mchakato utabainishwa ili kusaidia nchi kutambua malengo ya elimu ambapo bado hayapo lakini pia, inapofaa, kuonyesha athari inayoweza kutokea ya COVID-19 katika vigezo vya kitaifa kadiri data inavyoibuka.

MCHORO WA 3:

Nchi mbili kati ya tatu zimeshiriki katika utaratibu wa kutambua vigezo teule vya Lengo la 4 la Maendeleo Endelevu

Uwiano wa nchi kulingana na waliowasilisha vigezo teule vya kitaifa vya Lengo la 4 la Maendeleo Endelevu kufikia Oktoba 2021



GEM StatLink: https://bit.ly/GEM2021_Summary_fig3
Vyanzo: UIS na timu za Ripoti ya GEM.
EU = European Union; CARICOM = Caribbean Community

COVID-19 IMEATHIRI MATARAJIO YA KUFIKIA LENGO LA 4 LA MAENDELEO ENDELEVU NA NJIA ZA KUFUATILIA MAENDELEO

COVID-19 ndilo janga kubwa zaidi kuwahi kuikumba mifumo yote ya elimu duniani kwa wakati mmoja. Shule zilifungwa kwa asilimia 28 ya siku na kufungwa kwa muda kwa asilimia 26 ya siku kati ya Machi 2020 na Oktoba 2021. Kilele kilifikiwa mnamo Aprili 2020 (asilimia 95). Kati ya Septemba 2020 na Agosti 2021, shule zilifungwa (shule yote au sehemu yake) kwa nusu ya siku za shule **(Mchoro wa 4)**. Nchi nyingi ziliainisha shule zao kuwa zimefunguliwa kwa muda hata wakati nyingi zilikuwa zimefungwa.

Takwimu rasmi za Lengo la 4 la Maendeleo Endelevu, sehemu kubwa ni za 2019 na zinaonyesha hali kabla ya janga. Tathmini ya UIS ya vitengo 129 vya mipango vya wizara ya elimu kati ya Juni na Septemba 2020 iligundua kuwa theluthi mbili ya vitengo hivyo vililazimika kuchelewesha ukusanyaji wa data au kuuahirisha hadi mwaka uliofuata wa masomo kwani uwezo wao wa kukidhi mahitaji ya kuripoti uliathiriwa kiasi au pakubwa. Usimamizi wa utafiti pia uliathiriwa sana wakati wa janga.

Baadhi ya mipango mikubwa ya utafiti wa kaya ilibadilishwa kuwa tafiti za simu. Lakini zaidi ya tafiti 25 zilizopangwa au ambazo tayari zilikuwa zinaendelea mnamo 2020 zilikabiliwa na ucheleweshaji wa kazi za nyanjani. Matokeo yatapaswa kuzingatia kwa uangalifu ni lini hasa kazi ya nyanjani ilifanywa na ikiwa shule za karibu zilikuwa zimefunguliwa wakati huo. Aidha, tathmini za kujifunza ziliathiriwa. Kwa mfano, awamu ya 2021 ya Mpango wa Tathmini ya Kimataifa ya Wanafunzi iliahirishwa kwa mwaka.

Wingi wa vyanzo, pamoja na tofauti katika mbinu, sampuli, muda na miktadha, inamaanisha kazi ya kukusanya masimulizi kuhusu athari za COVID-19 bado ni changamoto. Kutokana na kukosekana kwa takwimu za kiusimamizi, tafiti nchini Ethiopia, Ghana na Senegal zinatoa ushahidi wa mapema kwamba watoto wanarudi shuleni baada ya kufunguliwa, ingawa kuongezeka kwa viwango vya kurudia kunaweza kumaanisha kwamba kuacha shule kumeahirishwa.

Mambo mawili makuu yanayoibua wasiwasi ni athari za kuvurugika kwa masomo na usambazaji usio na usawa wa masomo hasi na athari zingine kwa wanafunzi zaidi wasiojiweza. Duniani kote ni mtoto mmoja tu kati ya watatu, na mmoja kati ya watoto sita maskini zaidi, aliyeweza kutumia mtandao wa intaneti. Kwa hivyo njia bora zaidi za kujifunza kutoka umbali zilitenga idadi kubwa ya wanafunzi, na juhudi za kupanua njia hizo zitaathiri usawa katika muda mfupi hadi wa kati. Matumizi ya programu za kujifunzia kupitia simu za mkononi, ambayo yaliangaziwa sana na vyombo vya habari, yalikuwa ndiyo njia ambayo haikutumiwa sana katika utafiti wa nchi sita za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Njia hii ilitumiwa na watoto wasiozidi asilimia 17 nchini Nigeria na asilimia 12 nchini Ethiopia na haikutumiwa na yeyote nchini Burkina Faso, Malawi, Mali na Uganda.

Athari juu ya kujifunza zitategemea muda wa kufungwa kwa shule, njia ya kujifunza kutoka mbali na kiwango cha msaada kwa wanafunzi, mambo ambayo yalitofautiana sana kati ya nchi na ndani ya nchi. Tafiti nyingi zimefanyika katika nchi za kipato cha juu. Kwa kuzingatia wastani wa zaidi ya nchi saba, kupoteza katika kujifunza kulikuwa sawa na asilimia 30 ya mwaka wa masomo kwa hisabati na asilimia 35 kwa kusoma, kwa wastani, ikiwa shule zilifungwa kwa wiki nane. Lakini nchini Ufaransa, matokeo katika kusoma na hisabati yaliimarika miongoni mwa wanafunzi wa darasa la 6.

Kuna ushahidi bayana kwamba athari zinatofautiana kulingana na hali ya kijamii na kiuchumi. Nchini Marekani, uchambuzi wa viwango vya kufaulu katika mitihani ya wanafunzi wa darasa la 3 hadi 8 katika majimbo 12 ulionyesha kuwa kuhama kutoka masomo ya ana kwa ana hadi mfumo mseto au wa mtandaoni kulizidisha athari hasi kwa wastani wa pointi asilimia 10 katika hisabati na pointi asilimia 4 katika Kiingereza. Kubadilisha kwenda katika mfumo mseto au wa mtandaoni kumepunguza viwango vya kufaulu kwa pointi asilimia 4 kwa wilaya isiyo na wanafunzi Weusi au Wahispania lakini kwa pointi asilimia 9 kwa wilaya yenye asilimia 50 ya idadi ya wanafunzi Weusi na Wahispania.

Kuna upungufu wa tathmini za moja kwa moja za kujifunza katika nchi za kipato cha chini na cha kati. Huko São Paulo, Brazil, wanafunzi wa shule za sekondari walijifunza tu asilimia 27.5 ya kile ambacho wangejifunza shuleni kama hakungekuwa na janga; wanafunzi ambao shule zao zilifunguliwa walipata viwango vya chini vya kupoteza katika kujifunza. Nchini Kolombia, wanafunzi walitimiza alama tano chini ya mwaka uliopita, kiwango kinachowakilisha robo moja ya mwaka wa shule. Nchini Afrika Kusini, wanafunzi wa darasa la 2 na 4 walipoteza kati ya asilimia 57 na asilimia 81 ya mwaka wa ujuzi wa kusoma mnamo 2020, ikilinganishwa na wenzao wa kabla ya janga.

Tathmini za Ripoti ya kila Mwaka ya Hali ya Elimu zinazoongozwa na raia huko Asia Kusini zinaonyesha kuwa viwango vya kujifunza vimepungua katika madarasa ya mapema. Katika jimbo la Karnataka, India, asilimia ya wale walioweza kusoma maandishi ya darasa la 2 walitoka miongoni mwa wanafunzi wa madarasa yote lakini walipungua zaidi katika wanafunzi wa darasa la 4 (kutoka asilimia 33 hadi asilimia 18) kati ya 2018 na 2020. Nchini Pakistan, utafiti wa wilaya 16 uligundua kupoteza sawa kwa kujifunza katika ujuzi wa msingi katika darasa la 1 na la 3 lakini sio katika darasa la 5.

Ushahidi huu tofauti, ukichanganywa, unathibitisha kuwa kufungwa kwa shule kulikuwa na athari hasi kwa masomo ya wanafunzi. Ikiwa kupoteza kumefafanuliwa kwa misingi ya viwango vya chini vya ustadi vya Lengo la 4 la Maendeleo Endelevu, athari inaweza kuwa kubwa katika nchi za kipato cha kati kuliko nchi za kipato cha chini, ambapo viwango vya awali vilikuwa chini sana, au katika nchi za kipato cha juu, ambapo shule zilikaa zikiwa zimefungwa kwa muda mfupi na wanafunzi walipata fursa zaidi ya kujifunza mtandaoni. Bado, vipengele vingi havijulikani, ikiwemo kama viwango vya kujifunza vitarejea vilipokuwa au COVID-19 itakuwa na athari ya muda mrefu katika kujifunza.

Ili kupunguza matokeo, nchi zimeongeza au kurekebisha mwaka wa masomo na zimepatia kipaumbele maeneo fulani ya mtaala au ujuzi fulani. Theluthi mbili ya nchi ziliripoti kutekeleza hatua za kurekebisha katika elimu ya msingi na sekondari. Huko Ufilipino, Idara ya Elimu ilitoa mwongozo wa madarasa ya marekebisho ya wiki sita yaliyolenga wanafunzi ambao walipata alama chini ya asilimia 75 kwenye majaribio ya mwisho wa mwaka. Mpango wa Kitaifa wa Ukufunzi nchini Uingereza unatoa kozi za mafunzo ya saa 15 kwa wanafunzi milioni 6 wasiojiweza.


Janga hili pia limeleta changamoto ambazo hazijawahi kutokea **kwa walimu**. Kufungwa kwa shule kulipata walimu wengi wakiwa hawako tayari kuhamia kwenye mbinu za masomo ya mbali, wakiwa hawana uhakika kuhusu wajibu wao na wakiwa hawafahamu teknolojia. Katika utafiti wa zaidi ya walimu 20,000 katika nchi 165, asilimia 39 walisema kuwa ustawi wao wa kimwili, kiakili na kihisia ulikuwa umetatizika wakati wa janga hili. Kwa upande mwingine, asilimia 50 ya wahojiwa walisema kwamba walihisi shauku zaidi juu ya wito wao. Mgogoro huo umeibua maswali juu ya mabadiliko yanayohitajika katika maudhui ya kufundisha walimu. Zaidi ya maarifa ya kiteknolojia, walimu wanahitaji kushughulikia mahitaji mapya ya wanafunzi ya kijamii na kihisia na kitaaluma.

Elimu ya **maendeleo endelevu** na **uraia wa ulimwengu** ni jibu kwa changamoto za sayari ambayo inazidi kushikamana lakini ambayo mustakabali wake uko hatarini. Hata hivyo COVID-19 imeonyesha kushindwa kwa mifumo ya elimu kufuata maadili ya mshikamano na umoja wa nchi nyingi, na kuongezeka kwa ukosefu wa usawa ndani na kati ya nchi kunaibua wasiwasi wa kimaadili. Ulimwengu umeshuhudia hatua nyingi zilizo kinyume, kuanzia utaifishaji wa chanjo

MCHORO WA 4:

Zaidi ya miezi 20, shule zilikuwa zimefungwa kwa kiwango fulani kwa angalau asilimia 55 ya siku

Uwiano wa siku kwa kuzingatia hali ya kuwa zimefunguliwa, kwa mwezi, Februari 2020 hadi Oktoba 2021



GEM StatLink: https://bit.ly/GEM2021_Summary_fig4
Chanzo: UIS (2021c).

hadi sera za ubaguzi wa rangi na kuenea kwa imani baguzi. COVID-19 pia imemulika suala la elimu ya afya.

Athari halisi ya kufungwa na kufunguliwa kwa shule kwa mwelekeo wa maambukizi katika jamii bado haijabainika. Lakini kupunguza hatari ya maambukizi katika **mazingira ya kujifunzia** kunawezekana kupitia hatua kuanzia kuvaa barakoa, kudumisha umbali na kunawa mikono hadi kuonya dhidi ya kushiriki vitu na kunyunyiza kiua viini kwenye sehemu zinazoguswa mara kwa mara. Ufumbuzi usiotegemea teknolojia, wa kuboresha upitaji wa hewa ni pamoja na kutumia nafasi za nje na kufungua madirisha, ambapo msimu unaruhusu. Chini ya asilimia 10 ya nchi za kipato cha chini ziliripoti kwamba zilikuwa zimechukua hatua za msingi za kutosha kama sabuni ya kutosha, maji safi, barakoa, na vistawishi vya usafi ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi na wafanyakazi wote; nchi za kipato cha juu zilikuwa asilimia 96.

Ushahidi fulani unajitokeza kwamba janga hili na athari zake za baadaye zitakuwa zimepunguza ufadhili wa elimu kupitia mseto wa kupungua kwa mapato ya serikali na kuongezeka kwa mahitaji katika sekta zingine. Takwimu zilizokusanywa na UIS katika nchi 71 zinaonyesha kuwa mgao wastani wa elimu katika matumizi ya jumla ulipungua kutoka asilimia 14.1 mnamo 2019 hadi asilimia 13.5 mnamo 2021.

Katika **elimu ya chekechea**, hata mahali ambapo masomo ya mbali yalipatikana, changamoto zilijumuisha ukosefu wa mafunzo ya walimu, kurekebisha mafunzo ya mbali ili kuwafaa watoto wadogo, kufuatilia na kutathmini ukuaji wa watoto na kukabiliana na mazingira duni ya nyumbani ambapo hamna usaidizi wa kutosha. Kufungwa kwa shule na ushirikiano finyu ulinyima watoto vichocheo vya kijamii na kisaikolojia vinavyopatikana nje ya nyumbani mwao.

Elimu na mafunzo ya kiufundi yaliathirika kwani hadi asilimia 80 ya masomo yanahusu ustadi wa kutangamana na ule unaohitaji utekelezaji, ambazo zinapaswa kufundishwa watu wakiwa pamoja katika hali halisi. Kuandaa walimu limekuwa tatizo kubwa, kwani hawana uwezo wa kutoa mafunzo ya mbali, na mipango yao ya kawaida ya elimu ilivurugwa. Ni muhimu kutumia njia mbalimbali na kutotegemea tu suluhisho za teknolojia ya hali ya juu kutoa mafunzo ya mbali. Wakati huo huo, kuna mifano ya ustahimilivu ambapo mafunzo yanaendelea kusaidia sekta zilizoathirika sana.

Mafunzo ya mbali yalifanyika zaidi katika **Elimu ya juu** kuliko katika viwango vingine vya elimu. Katika utafiti wa nchi 53, 3 ziliripoti kuwa zimebadili kabisa na kuanza kufanyia masomo mtandaoni katika elimu ya juu, 19 zilikuwa na njia msingi za mtandaoni na 28 zilitumia njia mseto za masomo ya mbali na ya ana kwa ana. Nchi za kipato cha kati, kuanzia Kolombia hadi Misri na Uchina hadi Shirikisho la Urusi, zilibuni majukwaa ya mtandaoni. Lakini katika utafiti wa wanafunzi wa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ni asilimia 39 tu waliokuwa katika taasisi zinazotoa machaguo ya masomo ya mbali. Katika nchi za Umoja wa Ulaya, asilimia 41 ya wanafunzi ambao walifanya kazi na kusoma kwa wakati mmoja walipoteza kazi zao, asilimia 29 kwa muda na asilimia 12 kabisa.

Maeneo ya kimataifa yanayotumia Kiingereza, maarufu kwa wanafunzi, kama vile Australia, Nyuzilandi, Uingereza na Marekani yalikuwa na idadi ndogo ya **wanafunzi walioenda mle**. Huku hadi thuluthi moja ya wanafunzi nchini Australia wakiwa wa kimataifa, suala hili liliweka taasisi za elimu ya juu katika hatari kubwa ya kifedha. Wanafunzi na wahitimu walikuwa wamekwama katika nchi walimokuwa wameenda wakati walipokuwa wanatarajia kurudi katika nchi zao.

Elimu ya watu wazima ya ujuzi wa kusoma, kuandika na kuhesabu ni muhimu kwa elimu ya afya na kampeni za chanjo zenye ufanisi, na lazima iwe sehemu muhimu ya hatua za dharura za umma na mipango ya kujenga upya. Nchini India, wanawake walioshiriki katika mpango wa watu wazima wa kusoma na kuandika walikuwa na ufahamu wa juu zaidi wa COVID-19 kuliko wenzao wasiojua kusoma na kuandika. Ujuzi wa kuhesabu kilikuwa kiashiria thabiti zaidi wa uwezekano wa chini wa kuamini habari potofu kuhusu COVID-19. Lakini hata kabla ya janga, elimu ya mbali haikuwa inatumika sana katika utoaji wa mipango ya mwanzo ya kusoma na kuandika. Nchini Brazil, sheria fulani ilibainisha kuwa madarasa yanayolingana na mtaala wa msingi yalipaswa kuwasilishwa ana kwa ana.

LENGO LA 4.1. ELIMU YA MSINGI NA YA SEKONDARI

Kabla ya janga hili, watoto milioni 260, vijana wa umri wa shule za msingi na sekondari hawakuwa shuleni. Takwimu hiyo ilikuwa haijabadilika kwa mwongo mmoja. Mradi wa ushirikiano kati ya Ripoti ya GEM na taasisi ya UIS unafanywa ili kuunganisha na kugawanya vyanzo vya utafiti wa usimamizi na kaya, kujaza mapengo katika data ya usimamizi na kuendeleza mfululizo thabiti wa wakati. Mradi huu unaendeleza kazi ya timu ya Ripoti ya GEM na kuunganisha vyanzo mbalimbali ili kukadiria kiwango cha kumaliza shule. Tovuti mpya, VIEW (www.education-estimates.org) , inafanya iwe rahisi kwa njia hii kufikiwa na nchi. Viwango vya kumaliza elimu ya msingi vinakaribia au kuzidi asilimia 90 katika maeneo yote isipokuwa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambapo ni watoto wawili tu kati ya watatu wanaomaliza shule ya msingi. Hata hivyo, kiwango hicho kinaongezeka kutoka asilimia 65 hadi asilimia 76 ikiwa wale waliofikia daraja la mwisho wakiwa wamechelewa sana watajumuishwa **(Mchoro wa 5)**. Katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, asilimia 23 ya watoto katika shule za msingi na asilimia 31 ya vijana katika vidato vya chini vya shule za sekondari wamepitisha sana umri unaostahili, hivyo kuelezea kwa nini eneo hilo ndilo lenye pengo kubwa zaidi kati ya viwango vya kumaliza shule na kumaliza kwa wakati.

Katika kundi la kimataifa la nchi zilizojumuishwa katika utafiti wa Mielekeo ya Kimataifa katika Masomo ya Hisabati na Sayansi (TIMSS), wastani wa ongezeko la kila mwaka la kati ya 2015 na 2019 katika idadi ya wanafunzi waliofikia kiwango cha chini cha ustadi ilikuwa pointi asilimia 0.3 katika daraja la 4 na pointi asilimia 0.5 katika daraja la 8. Nchi zilizozidi wastani huu ni pamoja na Chile, ambapo idadi iliongezeka kutoka asilimia 41 mnamo 2003 hadi asilimia 57 mnamo 2011 na asilimia 70 mnamo 2019, yaani kiwango chake cha kuongezeka kilikuwa angalau mara tatu zaidi ya wastani. Kwingineko, kama katika nchi za Jordan na Romania, hakukuwa na ongezeko lolote au lilikuwa ndogo. Kufikia asilimia 10 ya mwisho ni changamoto hata katika mazingira yaliyo na rasilimali za kutosha. Nchini Marekani, asilimia 86 ya wanafunzi walifikia alama ya chini ya kimataifa ya TIMSS mnamo 1995 na asilimia 87 mnamo 2019; nchini Nyuzilandi, idadi hiyo iliendelea kupungua kutoka asilimia 89 mnamo 1995 hadi asilimia 82 mnamo 2019.


LENGO LA 4.2. ELIMU YA CHEKECHEA

Takwimu kuhusu Kielezo cha Maendeleo ya Utotoni kwa watoto wenye umri wa miezi 36 hadi 59 zinaonyesha kuwa pengo la utajiri lilidorora au likaongezeka. Mbinu ya kiashiria hiki, ambayo inaonyesha asilimia ya watoto wadogo wanaoendelea ifaavyo kiafya, katika kujifunza

MCHORO WA 5:

Kiashiria cha kumaliza shule kwa wakati unaofaa kinapunguza sana idadi ya watoto ambao hatimaye humaliza shule, hasa katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kiwango cha kumaliza shule hatimaye na kumaliza kwa wakati unaofaa, kulingana na eneo, 2000–20



GEM StatLink: https://bit.ly/GEM2021_Summary_fig5

Chanzo: Uchambuzi wa data ya utafiti wa kaya wa timu ya Ripoti ya GEM.

na ustawi wa kisaikolojia, imesasishwa kabisa. Kujifunza kunaanzia nyumbani. Mnamo 2012-19, asilimia 62 ya watoto walihusishwa katika shughuli nne au zaidi na mtu mzima katika kaya katika kundi la nchi za kipato cha chini na cha kati. Kiwango hiki kilikuwa chini ya asilimia 20 katika Gambia, Sierra Leone na Togo. Kikwazo muhimu katika kuchochea shughuli kama vile kusoma kwa pamoja ni upatikanaji wa vitabu. Kwa wastani, chini ya robo ya watoto wa chini ya miaka 5 walikuwa na angalau vitabu vitatu nyumbani. Katika nusu ya nchi, ni chini ya mtoto 1 kati ya 10 walionavyo; katika nchi 8 za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ni chini ya asilimia 1 ya watoto walionavyo.

Haki ya kupata elimu huanza wakati wa kuzaliwa. Wakati mtoto anapofikia umri wa miaka 3, asilimia 90 ya ubongo wake huwa umekomaa. Kushiriki kwa watoto wa chini ya miaka 3 katika mipango ya utunzaji na elimu ya chekechea huwa finyu, ingawa inafikia zaidi ya asilimia 20 kwa walio na miaka 0 hadi 1 na zaidi ya asilimia 60 kwa walio na miaka 2 katika nchi kadhaa za kipato cha kati na cha juu. Hata katika nchi zenye kipato cha juu, upatikanaji wa huduma za utunzaji na elimu ya chekechea bado unategemea sana historia ya kijamii na kiuchumi. Nchini Ufaransa na Ayalandi, tofauti ya ushiriki kati ya watoto wa miaka 0 hadi 2 katika kaya maskini na tajiri ni zaidi ya pointi asilimia 50. Duniani kote, asilimia 75 ya watoto waliandikishwa katika elimu ya chekechea mwaka mmoja kabla ya umri rasmi wa kujiunga, katika mwaka wa masomo uliokamilika 2020. Kiwango halisi cha uandikishaji kilichorekebishwa cha nchi za kipato cha chini kilikuwa nusu (asilimia 45) ya kile cha nchi za kipato cha juu (asilimia 91).


LENGO LA 4.3. ELIMU YA KIUFUNDI, YA JUU NA YA WATU WAZIMA

Elimu ya TVET bado haina ufadhili wa kutosha na mara nyingi hupuuzwa katika nchi nyingi, ingawa nchi zikiwemo Armenia, Brazil, Burundi, Kostarika, Indonesia na Urugwai zimeongeza viwango vya ushiriki katika miaka 15 iliyopita. Elimu ya sekondari ya ufundi huenda isionekane kuwa chaguo la kuvutia ikiwa, tofauti na cheti cha jumla cha sekondari, hakuna diploma ya ufundi inayotoa fursa ya kuendelea moja kwa moja katika elimu ya juu, kama ilivyo katika robo ya nchi. Kwa upande mwingine, katika asilimia 30 ya nchi, wahitimu wote wa shule za sekondari za ufundi

MCHORO WA 6:

Data ya uandikishaji katika elimu ya juu huenda ikaongeza au kupunguza idadi halisi ya waliohudhuria

Uwiano wa jumla wa waliohudhuria na waliojiandikisha katika elimu ya juu, 2015–19



GEM StatLink: https://bit.ly/GEM2021_Summary_fig6
Chanzo: Hifadhidata ya UIS.

wanafurahia fursa ya moja kwa moja ya kupata elimu ya juu.

Uwiano wa jumla wa uandikishaji katika elimu ya juu ulikuwa asilimia 39, na umeendelea kuongezeka kwa wastani wa karibu asilimia 1 kwa mwaka tangu 2000. Data hii ya kiusimamizi haikubaliani wakati wote na data ya utafiti juu ya mahudhurio **(Mchoro wa 6)**. Uandikishaji unaweza kupunguza mahudhurio ikiwa wanafunzi wengi wanahudhuria taasisi ambazo hazihesabiwi katika takwimu rasmi kwa sababu hazijatambuliwa au hazina idhini rasmi. Kwa upande mwingine, uandikishaji unaweza kuongeza mahudhurio ikiwa wanafunzi wengi wameandikishwa kwa majina tu, hasa ambapo masomo ni bure na hali ya kuwa mwanafunzi huja na nafasi za kupata huduma zenye ruzuku. Pia, data ya kiusimamizi inahusiana na umri wa kawaida wa miaka mitano inayofuata umri wa juu wa kuhitimu sekondari, lakini ni kawaida kujiandikisha kupata elimu ya juu mtu akiwa na umri wa juu zaidi, hasa katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Uwezo wa kumudu elimu ya juu kwa mtazamo wa maisha haufanyi elimu hiyo kuonekana ikiwa ya bei nafuu moja kwa moja. Hoja ya kiuchumi ya kugawana gharama katika elimu ya juu inategemea sana washiriki wanaotarajiwa ambao hawakabiliwi na vikwazo vya mkopo. Mikopo ya wanafunzi ya aina mbalimbali inapatikana katika nchi zaidi ya 70 na imeongezeka na kuwa soko la dola trilioni. Katika nchi nyingi, uwiano wa mapato ya wakopaji yanayohitajika kulipa mikopo ya wanafunzi ni mkubwa kupita kiasi, hasa kwa wahitimu wasio na uwezo mzuri wa kujimudu maishani. Marekebisho bora zaidi ya sera yamehusisha mabadiliko kutoka kwa mikopo inayotumika sana ya kulipa kulingana na wakati hadi mikopo inayozingatia mapato.

Katika nchi nyingi za kipato cha juu, waajiri ndio watoaji wakubwa zaidi wa elimu na mafunzo ya watu wazima. Hoja hii inaonyesha hitaji la sera zitakazolenga watu ambao wako nje ya soko la ajira. Hata kwa wale walioajiriwa, wakati wa kupata mafunzo unaweza kuwa na umuhimu sawa na udhamini, hivyo kuonyesha haja ya serikali kuchukua hatua kwa kutoa mipango ya likizo ya elimu. Takwimu za muda mrefu kutoka nchi sita za kipato cha juu zinaonyesha kuwa elimu ya watu wazima ni harakati ya mara kwa mara kwa wachache, hasa miongoni mwa walioelimika zaidi.

LENGO LA 4.4. UJUZI WA KAZI

Katika nchi 10 pekee kati ya 91 zenye data ndipo idadi kubwa ya watu wazima wanaripoti kuwa na angalau aina 5 kati ya 9 za ujuzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) unaofuatiliwa kwa ajili ya ulinganisho wa kimataifa. Katika karibu nusu ya nchi, idadi kubwa ya watu wazima hawana ujuzi wowote. Katika nchi nyingi za kipato cha chini na cha kati, ni vijana wachache ambao hawajamaliza angalau vidato vya chini vya sekondari walio na ujuzi wowote wa TEHAMA. Nchini Iraq, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao na Sierra Leone, hata walioelimika zaidi wana wastani wa chini ya aina mbili za ujuzi huu kati ya aina tisa. Upatikanaji wa vifaa na mtandao ni kikwazo kingine: Hata miongoni mwa walio na miaka 20 hadi 24, asilimia 98 ya wanawake na asilimia 90 ya wanaume nchini Chad waliripoti kuwa hawajawahi kutumia intaneti; viwango husika vilikuwa asilimia 61 na asilimia 63 katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Lao na asilimia 36 na asilimia 31 nchini Tunisia.

Mbinu ya kuwazia masuala kwa ruwaza sawa na kompyuta zinajumuishwa katika mitaala ya kitaifa. Nchi ya Ufini imefanya masomo ya algorithi na usanifu wa programu ya lazima kutoka darasa la 1 kama sehemu ya fani mbalimbali za mtaala. Katika ukaguzi wa nchi nane za kipato cha juu mnamo 2018, wanafunzi ambao mara nyingi walitumia TEHAMA shuleni kwa kazi zinazohusiana na shule hawakupata alama ya juu kuliko wenzao, na wanafunzi walio na uzoefu wa kusanifu programu hawakuweza kutumia ujuzi huo katika mazingira yasiyohusisha usanifu wa programu.

Ujuzi wa kifedha ni muhimu kwa maisha katika uchumi wa kisasa na katika maisha ya utu uzima kwa ujumla, lakini sio kila mtu aliye na nafasi ya kujifunza dhana muhimu za kifedha shuleni. Programu ya 2018 ya Tathmini ya Kimataifa ya Wanafunzi ilijumuisha moduli ya hiari ya ujuzi wa kifedha, ambayo ilitumiwa na mifumo 20 ya elimu iliyoshiriki. Wasichana walikuwa na uwezekano mdogo wa kuripoti shughuli za darasani zinazohusiana na mada za kifedha katika nchi zote zilizoshiriki, licha ya ukweli kwamba elimu ya kifedha kwa kawaida hujumuishwa katika hisabati, somo ambalo kwa jumla ni la lazima.

LENGO LA 4.5. USAWA

Ukosefu wa usawa wa kijinsia bado ni kero kuu, hata kama kuelewa changamoto mbalimbali katika ngazi tofauti na katika maeneo tofauti kunahitaji uwezo wa kuelewa tofauti ndogo ndogo zilizopo. Elimu ya sekondari ya vidato vya juu ndiyo ngazi ambapo wasichana balehe wanaweza kukabiliwa na hali ngumu (k.m. nchini Benin, Chad na Niger), lakini pia wana uwezekano wa kufurahia faida na mabadiliko ya haraka katika hali, yatakayowafaa. Jambo hili linatokea katika nchi mbalimbali, zikiwemo zile ambazo ziko mbali zaidi katika kufikia lengo la 4 la Maendeleo Endelevu

ikilinganishwa na wenzao katika maeneo mahususi, ikiwa ni pamoja na Kambodia, Kongo, Gambia, Ghana, Malawi na Rwanda.

Mali, ambayo hupimwa katika ngazi ya kaya, hayaonyeshi kila wakati hali za kunyimwa zinazowapata watoto. Katika nchi kadhaa, asilimia 10 ya watoto wanaonyimwa nafasi za masomo wako katika kaya tajiri zaidi, na zaidi ya asilimia 30 ya watoto katika kaya maskini zaidi hawanyimwi nafasi hizi. Kiwango cha kumnyima mtoto nafasi za masomo kinaweza kuwa utabiri thabiti wa ziada wa matokeo ya elimu.

Idadi kubwa ya watoto wanahudhuria shule zinazodhibitiwa na vikundi vyenye silaha visivyo vya serikali. Vikundi hivi vina sababu nyingi za kuchagua kutoa elimu, iwe kupitia udhibiti wa moja kwa moja, hatua teule, k.m. katika mtaala, au kuwaacha watoa huduma waliopo waendelee kufanya kazi. Elimu ni miongoni mwa huduma zenye thamani kubwa zinazohitajika na raia; kushindwa kuitoa kunaweza kusababisha chuki.

Kuna changamoto za utofauti wa lugha katika elimu. Katika nchi za magharibi na kati mwa Afrika, ikiwemo Chad, Gambia na Togo, watoto wenye umri wa miaka 7 hadi 14 wanaozungumza lugha ya kufundishiwa wakiwa nyumbani hawazidi asilimia 5. Mbinu inayoleta pamoja sera ya lugha ya kufundishia na vyanzo vya data vya lugha, makadirio ya idadi ya watoto wenye umri wa kwenda shule na viwango vya uandikishaji ilionyesha kwamba asilimia 37 ya watoto katika nchi za kipato cha chini na cha kati walijifunza katika lugha nyingine kando na wanayotumia nyumbani: asilimia 27 walizungumza lugha ya maandishi ya wachache na asilimia 10 walizungumza lugha isiyo ya kawaida, kila mmoja ikiwa na wazungumzaji wachache.

LENGO LA 4.6. KUJUA KUSOMA, KUANDIKA NA KUHESABU

Ulimwenguni, kati ya watu wazima wenye umri wa miaka 15 na zaidi, asilimia 83 ya wanawake na asilimia 90 ya wanaume wanajua kusoma na kuandika, kwa kuzingatia uainishaji wa watu wanaoweza kusoma na kuandika katika makundi mawili; pengo la pointi asilimia 7. Zaidi ya mmoja kati ya vijana wanne wa kike hawajui kusoma na kuandika katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambapo viwango vya kusoma na kuandika miongoni mwa vijana wa kike vimeongezeka kwa chini ya asilimia moja kwa mwaka. Kote duniani, kushuka kwa idadi ya wanawake wasiojua kusoma na kuandika katika Asia ya Mashariki na Kusini-Mashariki kumeghairiwa na ongezeko la idadi ya wanawake wasiojua kusoma na kuandika katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Isitoshe, dhana kwamba wote waliomaliza masomo ya sekondari wanajua kusoma na kuandika inamaanisha kuwa makadirio halisi ya wanaojua kusoma na kuandika ya hapo awali yamekuwa yakiongezwa kupita kiasi. Karibu nusu ya waliomaliza vidato

MCHORO WA 7:

Hata waliomaliza masomo ya sekondari hawawezi kuchukuliwa kuwa wanaweza kusoma na kuandika

Viwango vya kuweza kusoma na kuandika katika kikundi cha umri wa 20 hadi 24, kulingana na kiwango cha masomo, baadhi ya nchi, 2015–19



Kumbuka: Ukubwa wa kitone unaambatana na ukubwa wa idadi ya watu katika kila kiwango cha masomo.

GEM StatLink: https://bit.ly/GEM2021_Summary_fig7

Chanzo: Uchambuzi wa timu ya Ripoti ya GEM wa data ya DHS.

vya chini vya sekondari katika nchi 18 zilizo na data ya utafiti wa hivi karibuni hawafikii kiwango cha msingi cha ujuzi wa kusoma na kuandika, kinachofafanuliwa kama kuweza kusoma sentensi rahisi **(Mchoro wa 7)**.

Ukweli unaopingana, kwamba kutoenda shule hakumaanishi kuwa mtu hana ujuzi wa kusoma na kuandika, unaangazia umuhimu wa kupata uwezo wa kusoma na kuandika nje ya shule. Kuhusiana na makadirio ya idadi ya watu wasiojua kusoma na kuandika, uandikishaji wa watu wazima katika programu zisizo rasmi za ISCED 1 ni asilimia 1 au chini yake nchini Bolivia, Hondurasi, Msumbiji, Qatar na Suriname, asilimia 2 nchini Bahrain na Peru, asilimia 3 nchini Kolombia na Thailand, asilimia 4 nchini Saudia na asilimia 8 katika Jamhuri ya Dominika.

Takwimu hata kuhusu ujuzi rahisi wa kuhesabu ni haba. Kipimo mbadala cha ujuzi msingi wa kuhesabu kinaweza kuhesabiwa kama asilimia inayoelezea umri wao kwa usahihi, ambayo inaonyesha uwezo wa kufanya kazi na nambari rahisi, za chini. Ingawa wengi, hata walio maskini zaidi, wanapita kiwango hiki, kipimo hiki kinafaa kwa kuchunguza mwenendo wa kihistoria wa ujuzi wa kuhesabu. Uchambuzi wa takwimu za utafiti wa kaya na sensa ya watu unaruhusu ujuzi wa kuhesabu wa watu waliozaliwa kati ya miaka ya 1960 na 2010 kufuatiliwa katika nchi 42 za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Maendeleo kadiri muda umepita yamekuwa finyu na hayajadumishwa miongoni mwa walio maskini zaidi. Karibu sehemu yote ya ongezeko la jumla la ujuzi wa kuhesabu barani Afrika ilitokana na kuongezeka kwa wanaoenda shule.

LENGO LA 4.7. MAENDELEO ENDELEVU NA URAIA WA KIMATAIFA

Lengo la 4.7 linaenda mbali zaidi kuliko ajenda zingine za Lengo la 4 la Maendeleo Endelevu katika kushughulikia kile wanafunzi wanahitaji kujifunza ili kufikia malengo yenye mabadiliko, ya Lengo la 4 la Maendeleo Endelevu. Sehemu ya shule zinazotoa elimu kuhusu VVU na ujinsia inayojikita kwenye stadi za maisha mara nyingi huwa chini, hasa katika ngazi ya msingi, k.m. asilimia 2.5 ya shule za msingi nchini Burkina Faso na asilimia 6 nchini Niger. Hata hivyo, Mwongozo Uliorekebishwa wa Kimataifa wa Kiufundi wa Umoja wa Mataifa kuhusu Elimu ya Ujinsia unapendekeza kufundisha masuala ya kubalehe na hedhi kabla ya wanafunzi kuzipata, yaani katika umri wa miaka 9 hadi 12. Zana ya Kutathmini na Kukagua Elimu ya Ujinsia ya UNESCO inasimamia ripoti ya hivi karibuni ya maendeleo ulimwenguni kuhusiana na elimu kamili ya ujinsia. Miongoni mwa nchi 24, ni nchi 3 tu zinazotathminiwa kuwa zinatoa maudhui ya mtaala ya 'kina' kuhusu afya ya ngono na uzazi kwa wenye miaka 9 hadi 12, na nchi 5 zina maudhui 'madhubuti'.

Utafiti wa Kimataifa wa Elimu ya Uraia uliofanywa 2016 katika nchi 23 za kipato cha kati-juu na cha juu uligundua kuwa asilimia ya wanafunzi wenye uelewa wa kutosha wa masuala yanayohusiana na uraia wa ulimwengu ni kati ya asilimia 40 katika Jamhuri ya Dominika, Latvia na Uholanzi na karibu asilimia 70 katika Korasia, Jamhuri ya Korea na Uswidi. Tathmini ya TIMSS ya 2019 ilionyesha kuwa ni takriban asilimia 30 pekee ya wanafunzi waliofikia ustadi katika ujuzi wa sayansi ya mazingira. Elimu ya mabadiliko ya tabianchi inalenga kusaidia watu kuelewa, kushughulikia, kupunguza na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Msururu mpya wa wasifu wa nchi juu ya mawasiliano na elimu ya mabadiliko ya tabianchi uliofanywa na Ripoti ya GEM na mradi wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Mawasiliano na Elimu kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi unatoa mtazamo linganishi. Seti ya kwanza ya wasifu 20 za nchi inajumuisha maeneo yote na vikundi vya nchi kulingana na mapato. Seti ya pili ya hadi wasifu 50 imepangwa kuchapishwa mwaka 2022. Uchambuzi wa awali unaonyesha kuwa uzingatiaji wa mabadiliko ya tabianchi ulipatikana katika asilimia 40 pekee ya sheria za elimu za kitaifa na asilimia 45 ya mipango au mikakati ya sekta ya elimu..

LENGO LA 4.A. VISTAWISHI VYA ELIMU NA MAZINGIRA YA KUJIFUNZA

Kujifunza kwa ubora wa kiwango kizuri hakuwezi kufanyika ikiwa mazingira hayafai, hata zaidi ikiwa mazingira yanatishia ustawi wa watoto. Azimio la Shule Salama, ahadi ya kisiasa baina ya serikali ya kulinda wanafunzi, walimu, shule na vyuo vikuu dhidi ya mashambulizi wakati wa vita, sasa limeidhinishwa na nchi 112. Ushahidi unaoonyesha kwamba adhabu ya viboko haikiuki tu haki za watoto, bali pia inaathiri matokeo ya elimu, unaendelea kuongezeka. Adhabu ya viboko sasa imepigwa marufuku kabisa shuleni katika nchi 156.

Shule inaweza kuwa mahali pekee ambapo watoto wengine wanapata maji, mazingira na vistawishi vya usafi. Nchini Liberia, ni kaya chache tu zilizo na vistawishi vya usafi ambavyo vinakidhi kiwango cha msingi cha kimataifa, lakini asilimia 69 ya shule zina vistawishi hivyo. Hata hivyo, shule ndogo, hasa zilizoko katika maeneo ya mbali na vijijini, zinaweza kuchukuliwa kuwa zenye uwezekano mdogo wa kukidhi vigezo vya ubora wa miundombinu ikilinganishwa na shule kubwa. Nchini Cabo Verde, asilimia 22 ya shule za msingi mnamo 2018 hazikuwa na istawishi vya msingi vya kunawia mikono. Hata hivyo, idadi ndogo zaidi ya asilimia 22 ya shule za msingi zilichangia asilimia 2 tu ya uandikishaji

wa shule za msingi. Kote duniani, kiwango cha watoto wanaohudhuria shule zisizo na vistawishi vya msingi kwa hivyo, ni cha chini sana kuliko kiwango cha shule.

Zaidi ya vistawishi halisi, mambo mengine kama vile mpangilio wa kalenda za shule – kuanzia uratibu wa siku za kufundisha katika wiki na miaka hadi muda na mpangilio wa siku yenyewe ya shule - yanaweza kuwa na matokeo muhimu katika ubora na usawa wa mifumo ya elimu. Muundo wa kalenda ya shule katika nchi nyingi unatokana zaidi na ushawishi wa historia ya ukoloni kuliko misimu, na hauendani vizuri na misimu ya kilimo ya eneo husika. Nyakati za kuanza shule pia ni muhimu. Mbali na kuruhusu muda zaidi wa kulala, kuanza baadaye kunaonekana kuambatana vizuri na utaratibu wa kimwili wa saa 24 wa vijana, na viwango vya juu vya umakinifu katika nyakati za baadaye za asubuhi na jioni.

LENGO LA 4.B. UFADHILI

Misaada ya jumla ya kusaidia usafiri wa wanafunzi iliongezeka kwa asilimia 30 kati ya 2015 na 2019, kutoka dola za Marekani bilioni 3.4 hadi dola za Marekani bilioni 4.4. Jumla ya misaada ya ufadhili kwa nchi za kipato cha chini iliongezeka maradufu kutoka 2015 hadi 2019, na kuzidi ukuaji wa uandikishaji katika elimu ya juu. Lakini kwa kuzingatia nchi zote za kipato cha chini na cha kati, idadi ya wanafunzi waliosafiri nje ilizidi kiwango cha kukua cha misaada ya ufadhili. Kwa wastani, kwa kila mwanafunzi wa kimataifa, kiwango cha misaada ya ufadhili kilikuwa chini katika 2019 ikilinganishwa na 2006. Takwimu zisizo linganifu zinazopatikana zinaonyesha kuwa lengo la upanuzi mkubwa katika ufadhili kufikia mwaka wa 2020 halijafikiwa. Lakini wafadhili sasa wana uwezekano zaidi wa kutoa ufadhili wa kimasomo kwa nchi zinazoendelea kuliko mwaka 2015, na la muhimu zaidi, uwezekano wa nchi zinazopokea ufadhili kutegemea mfadhili mkuu mmoja au wawili uko chini.

Dhana ya 'kuhama kwa wataalamu' (brain drain), ambapo wale waliopokea ufadhili hawarudi katika nchi zao za asili, imeanza kubadilishwa na uelewa wa kisasa zaidi wa 'kuenea kwa wataalamu' (brain circulation). Makadirio ya hivi karibuni yanaonyesha kuwa wahamiaji wanaorudi wanawakilisha sehemu kubwa ya watu wanaohamia kwenye nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na Amerika Kusini, na kwamba wahamiaji hawa wameelimika zaidi, kwa wastani. Nchi zingine zinatambua kwamba hata raia wake wenye ujuzi ambao hawatarudi nchini humo katika siku zijazo wana faida kubwa ikiwa watahusishwa ifaavyo. Kati ya nchi 22 za Amerika ya Kusini na Karibi zilizotathminiwa kwa ajili ya Kielezo cha Sera za Wahamiaji, 8 zinadumisha mitandao rasmi ya kuenea kwa wataalamu. Utambuzi wa awali wa sera za utawanyikaji za nchi 35, unaowakilisha maeneo yote duniani, madaraja ya mapato na aina za serikali, uligundua kuwa theluthi mbili ilidumisha aina fulani ya mitandao ya kisayansi na nusu iliweka masharti kwa wanafunzi waliofadhiliwa masomo nje ya nchi kurejea.

LENGO LA 4.C. WALIMU

Takwimu zilizoripotiwa zinaonyesha kuwa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ndilo eneo lenye asilimia ndogo zaidi ya walimu wanaofikia viwango vya kitaifa: asilimia 57 katika elimu ya chekechea (ikilinganishwa na asilimia 83 katika Amerika ya Kusini na Karibi), asilimia 67 katika shule za msingi (ikilinganishwa na asilimia 85 katika Afrika Kaskazini na Asia ya Magharibi) na asilimia 61 katika elimu ya sekondari (ikilinganishwa na asilimia 78 katika Asia ya Kati na Kusini). Kwa hivyo, uwiano wa wanafunzi na walimu waliohitimu ni karibu mara mbili zaidi katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kama wastani wa ulimwengu, licha ya kuboreka kidogo tangu 2015.

Hata walimu waliohitimu huenda wasiwe wamehitimu katika lile somo wanalofundisha. Katika sehemu nyingi za ulimwengu, suala la kufundisha somo tofauti na lile mwalimu alisomea limeenea. Katika angalau mifumo 40 ya elimu ambayo ilishiriki katika Utafiti wa Kimataifa wa Kufundisha na Kujifunza wa 2018, zaidi ya asilimia 10 ya walimu wa sayansi wa vidato vya chini vya shule za sekondari hawakuwa wamepata elimu rasmi au mafunzo katika somo hilo. Hali hiyo ilijitokeza kwa walimu wa hisabati. Nchini Georgia na Saudia, ni chini ya asilimia 60 ya walimu wa sayansi na hisabati waliopata mafunzo katika masomo yao kama sehemu ya elimu yao rasmi. Mwalimu kufundisha somo lingine kando na alilohitimu huibua wasiwasi wa usawa, kwani sio kila mtu ana uwezekano sawa wa kuwa, au kufundishwa na, mwalimu anayefundisha somo tofauti na alilohitimu. Jambo hili hujitokeza sana katika maeneo ya vijijini na shule zinazohudumia wanafunzi wasiojiweza sana.

Makadirio mapya ya UIS ya kiashiria cha mshahara wa mwalimu, yanayochunguza jinsi walimu wanavyoendelea ikilinganishwa na fani nyingine zinazohitaji kiwango kinachofanana cha kufuzu, yanaonyesha kwamba tofauti wastani kati ya walimu katika viwango tofauti vya elimu ndani ya nchi moja kwa ujumla ni ndogo ikilinganishwa na tofauti kati ya nchi. Katika nchi zenye kipato cha juu, ambapo ushahidi mwingi hutoka, walimu huwa wanalipwa kidogo kuliko wataalamu wanaolingana katika sekta zingine **(Mchoro wa 8)**.

Kiashiria cha mshahara wa mwalimu kinachukuliwa kama kiwakilishi cha motisha wa walimu. Lakini kuna mambo mengi zaidi yanayoathiri motisha, kama uchambuzi wa hivi karibuni wa kiwango cha juu cha walimu kutofika shuleni katika nchi nane za mashariki na kusini mwa Afrika unavyoonyesha. Hata kwa mujibu wa walimu wenyewe, sehemu ya wale waliokosa kufika shuleni angalau mara moja kwa wiki ni kati ya chini ya asilimia 10 nchini Kenya na Rwanda hadi karibu asilimia 30 nchini Sudan Kusini. Walimu wanasema kuwa wanakosa kufika kutokana na sababu za kiafya (asilimia 62) na kifamilia (asilimia 35), ikifuatiwa na hali ya hewa (hasa mvua kubwa na joto kali), shughuli rasmi za shule na matatizo ya usafiri.

ELIMU KATIKA MALENGO MENGINE YA MAENDELEO ENDELEVU


Upatikanaji wa nishati nyumbani unaweza kuchangia pakubwa katika kuruhusu watoto kushiriki katika shughuli za elimu. Mpango wa kuweka umeme vijijini kule Bhutan ulisaidia kupunguza matumizi ya kuni na kusababisha ongezeko la miaka 0.8 ya masomo, na athari kubwa zilikuwa kwa wasichana kuliko wavulana. Upatikanaji wa nishati shuleni unaweza kusaidia kuboresha mazingira ya kujifunzia na kupanua upatikanaji wa rasilimali za kujifunzia. Programu ya Msaada wa Usimamizi wa Sekta ya Nishati iligundua kuwa asilimia 72 ya shule nchini Kenya, na asilimia 22 tu nchini Ethiopia, ziliweza kupata nishati ya kitaifa ya umma. Barabara husaidia kupunguza umaskini na kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii, ikiwemo matokeo ya elimu. Katika eneo la Antioquia nchini Kolombia, barabara bora za vijijini zilihusishwa na utendaji bora katika elimu kwa wanafunzi wa vijijini

Katika juhudi za kujikaza kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu ifikapo 2030, kumekuwa na maendeleo ya kusifiwa katika kuboresha teknolojia ya nishati jadidifu, yanayoungwa mkono na uwekezaji mkubwa katika juhudi za kuanza kutumia nishati ya jua na upepo. Pia watu zaidi wanafahamu haja ya kutumia na kuzalisha kwa njia endelevu. Hata hivyo, uboreshaji katika maeneo ya malengo ambayo hayalengi soko – k.m. ufikiaji sawa wa teknolojia safi ya kupikia, utaalamu juu ya nishati jadidifu, msaada wa kifedha wa kuimarisha uwezo kwa nchi za kipato cha chini kabisa, maendeleo anuai na yenye usawa ya nguvukazi - umekumbwa na changamoto. Elimu inasaidia kufikia malengo endelevu. Taasisi za elimu

MCHORO WA 8:

Ikilinganishwa na taaluma zingine, walimu hulipwa mishahara ya chini katika nchi za kipato cha juu na mishahara ya juu katika baadhi ya nchi za kipato cha chini na cha kati

Mshahara wastani wa mwalimu ikilinganishwa na taaluma zingine zinazohitaji viwango sawa vya kuhitimu, miaka ya mwisho kupatikana 2015–19



GEM StatLink: https://bit.ly/GEM2021_Summary_fig8

Chanzo: Hifadhidata ya UIS.

zinahitaji kuboresha uelewa wa wanafunzi kuhusu nishati na changamoto nyingine za uendelevu. Uhamasishaji wa umma unaweza kuchangia mabadiliko mapana ya kijamii. Uimarishaji wa uwezo wa kitaaluma unahitaji kufanyika kwa kasi isiyo ya kawaida ili kuwezesha mabadiliko ya kuanza kutumia nishati jadidifu.

UFUATILIAJI WA FEDHA

Sehemu ya matumizi ya jumla ya umma inayochukuliwa na elimu iliongezeka kutoka asilimia 13.8 mwaka 2000 hadi asilimia 14.1 mwaka 2019. Takwimu za hivi karibuni za nchi 71 zinaonyesha kuwa kiwango hicho kilipungua hadi asilimia 13.5 mwaka wa 2021, ishara ya athari kali ya COVID-19. Kati ya nchi 151 zilizokuwa na takwimu za 2014-19, nchi 48, au asilimia 32, hazikufikia vigezo vyote viwili vya asilimia 4 ya Pato la Taifa na asilimia 15 ya matumizi ya serikali katika elimu. Baadhi ya nchi zinafaulu kabisa katika kuzindua programu ambazo zinawafikia wasiojiweza. Algeria hutoa ruzuku ya elimu ya mwaka, sawa na dola za Marekani milioni 23, kwa wanafunzi milioni 3 wa shule za msingi na sekondari: asilimia 38 ya wale masikini zaidi na asilimia 10 ya matajiri hupokea msaada.

Misaada kwa elimu ilisalia katika kiwango cha dola za marekani bilioni 15.3 mwaka wa 2019. Ufanisi wa misaada una maana tofauti kwa watu tofauti. Ufafanuzi mmoja unazingatia umiliki wa nchi na matokeo, uwazi na uwajibikaji wa pamoja, na ushirikiano wa maendeleo jumuishi. Sehemu ya msaada wa moja kwa moja wa bajeti katika misaada ya jumla ilishuka kutoka asilimia 6.6 mnamo 2002 hadi asilima 2.5 mnamo 2019.

Uchambuzi wa ripoti za utafiti wa bajeti za kaya kutoka nchi 100 za kipato cha chini na cha kati katika miaka ya 2010 uligundua kuwa elimu ilikuwa asilimia 3.2 ya matumizi ya jumla ya kaya, na kufikia asilimia 6 au zaidi nchini Haiti na Lebanon na katika nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, zikiwemo Rwanda, Uganda na Zambia.

Wahusika wasio wa serikali katika elimu:

NI NANI ANAYECHAGUA? NI NANI ANAYEPOTEZA?

Jukumu la wahusika wasio wa serikali linazidi utoaji wa masomo hadi hatua katika viwango mbalimbali vya elimu na nyanja za ushawishi. Pamoja na tathmini yake ya hatua zilizopigwa za kufikia lengo la 4 la Maendeleo Endelevu, ikiwemo ushahidi unaoibuka juu ya athari ya janga la COVID-19, Ripoti ya Ufuatiliaji wa Elimu ya Kimataifa ya 2021/2 inahimiza serikali kuona taasisi, wanafunzi na walimu wote kama sehemu ya mfumo mmoja. Viwango, maelezo, vichochezi na uwajibikaji vinapaswa kusaidia serikali kulinda, kuheshimu na kutimiza haki ya elimu kwa wote, bila kupuuza masuala ya upendeleo au unyonyaji. Si lazima elimu inayofadhiliwa na serikali itolewe na serikali, lakini lazima utofauti katika michakato ya elimu, matokeo ya wanafunzi na mazingira ya kazi ya walimu yashughulikiwe. Ufanisi na uvumbuzi unapaswa kuenezwa na kutekelezwa na wote, badala ya kusalia kama siri za kibiashara. Ili kufikia lengo hilo, uwazi na uadilifu katika mchakato wa sera ya elimu ya umma vinahitaji kudumishwa ili kuzuia masilahi binafsi.

Kauli mbiu ya ripoti – Ni nani anayechagua? Ni nani anayepoteza? – ni mwaliko kwa watunga sera kudadisi uhusiano na wahusika wasio wa serikali katika suala la machaguo ya msingi: kati ya usawa na uhuru wa kuchagua; kati ya kuhimiza uchukuaji hatua na kuweka viwango; kati ya vikundi vya uwezo na mahitaji tofauti; kati ya ahadi za sasa chini ya lengo la 4 la Maendeleo Endelevu na zile za kutimizwa hatua kwa hatua (k.m. elimu ya baada ya sekondari); na kati ya elimu na sekta zingine za kijamii.

Kuna zana mbili za mtandaoni zinazoambatana na ripoti ya tano ya *Ufuatiliaji wa Elimu Duniani*: PEER, rasilimali ya mazungumzo ya sera inayoelezea shughuli na kanuni zisizo za serikali katika mifumo ya elimu duniani; na VIEW, tovuti mpya inayojumuisha vyanzo na kutoa makadirio mapya ya kiwango cha kukamilika kadiri muda unavyopita.

unesco
Global Education Monitoring Report

4 QUALITY EDUCATION

Sustainable Development Goals

www.unesco.org/publishing • wwww.unesco.org/gemreport